**NGO** zapinga kifungu sheria kupambana na rushwa ngono

UKURASA 5

**ADAIWA** kujinyonga akiwa katika mahabusu ya mahakama

UKURASA 2



UKURASA 19

**HOMA YA NYANI:** Wizara yasema Watanzania wako salama, tahadhari yatolewa Afrika




UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Agosti 15, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581769

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Msajili, Kamishna Awadh kushtakiwa

**UKIMYA** watawala Jeshi la Polisi kujibu tuhuma dhidi yao...*Endelea ukurasa wa 2*



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu na Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Ugonjwa afya ya akili watesa kinamama baada ya kujifungua

UKURASA 4



## Profesa Janabi: Kufunga kula ni kinga dhidi ya maradhi

UKURASA 3

**MICHEZO** KMC YAWAITA SIMBA MEZANI KUMCHUKUA AWESU AWESU UK 23

MAONI, KATUNI UK.6

# Msajili, Kamishna Awadh kushtakiwa



CP Awadh Haji



Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wameeleza madhila waliyopitia wakiwa mikononi mwa polisi, huku wakitangaza kuwashtaki mahakamani Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza na Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, CP Awadh Haji.

Katika mkutano wao na waandishi wa habari kwenye ofisi za makao makuu ya chama hicho Kinondoni, Dar es Salaam jana, viongozi hao walidai walipigwa na polisi kwa marungu na vifa vya umeme, huku wakilazimishwa kupandishwa kwenye magari.

Vilevile, wamedai kuwa kabla ya kukamatwa mkoani Mbeya wiki iliyopita, ofisi yao ya jijini Mbeya ilizingirwa na askari wenye silaha walizoziita "nzito", wakatolewa lugha mbaya na kuvunjiwa miwani yao.

Viongozi hao ni Mwenyekiti, Freeman Mbowe, Makamu Mwenyekiti Bara, Tundu Lissu, Katibu Mkuu, John Mnyika na Mwenyekiti wa Baraza la Vijana (BAVICHA), John Pambalu.

Katibu Mkuu wa Chama hicho, John Mnyika alidai alipelekwa eneo lenye giza na kushushiwa kipigo kikali kisha kurushwa kwenye gari ambako alimkuta Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi 'Sugu' akiwa "amepewa kipigo kikali".

Mnyika pia alidai kuchukuliwa simu zao na askari waliopeleka vituo vya polisi katika mikoa ya Songwe, Njombe na Iringa huku wakipewa amri ya kulala kifudifudi kwenye bati la gari aina ya landcruizer.

**MBOWE**

Mwenyekiti wa CHADEMA, Mbowe, alisema chama chao si cha kigaidi, hivyo ameagiza wanasheria wa chama kukutana haraka kuandaa mashtaka dhidi ya Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Nyahoza na Kamishna Awadh.

"Ninawakumbusha tu Makamu wetu Mwenyekiti (Lissu) ambaye ni wakili ataongoza jopo hili. Kwa muda mrefu hatujamwona Lissu mahakamani, sasa tutamwona na leseni yake ya uwakili imesharejeshwa," alisema.

Mbowe pia alisema kuwa tangu warejeshe mikutano ya hadhara chama kimeifanya pamoja na maandamano na hawajawahi kumdhuru yeyote kwa kuwa si chama cha kigaidi, bali cha Watanzania.

"Hatuwezi kuwa chama cha kuadhibu wenye chama chao, hawa tutawawajibisha kama nilivyozungumza. Joseph Mbilinyi anaendelea na matibabu, alitamani kuja, yupo Dar es Salaam.

"Ni mgonjwa, jana (juzi) alilazwa Muhimbili, leo (jana) usiku akatoka, akarudishwa tena, wamemwumiza sana Kamanda Sugu kwa maelekezo ya Awadh," alidai Mbowe.

Mwenyekiti huyo pia alidai Kamishna Awadh alishiriki kuvunja miwani ya Katibu Mkuu Mnyika, akieleza kuwa viongozi wa CHADEMA wanabeba maumivu hayo kwa ajili ya taifa.

"Tunafanywa kondoo wa kafara si kwamba hatuna nyumba au vitanda vya kulala, tunatekeleza wajibu na wanachama muutekeleze.

"Kama tuna intelijensia katika nchi inayoweza kulichafua taifa zima matope, inatueleza tunaongozwa na watu wa namna gani. Hii operesheni imegharimu Jeshi la Polisi na nina hakika siwezi kusema kiasi, lakini yote tuliyoona mpaka kulipiwa nauli, watu kulipwa posho ni mamilioni ya walipakodi wa nchi hii.

"Hivi kweli fedha zetu sisi taifa maskini zinapaswa kutumika kwa mambo ya kihuni? Barua ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambayo ni chimbuko la uhuni wote huu, inasema kiongozi wetu Katibu Mwenezi BAVICHA, eti alizungumza maneno haya na ndio mwanzo wa sakata hili," Mbowe alilalama.

**LISSU**

Makamu Mwenyekiti Bara, Lissu alidai polisi walikwenda kivita katika ofisi zao za Kanda ya Nyasa, jijini Mbeya, wakiwa na silaha za moto, mabomu na fimbo za umeme.

Alisema kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga, aliingia ndani walimokuwa na kuwaeleza alitaka kuzungumza na viongozi.

"Tulimkaribisha, aliingia yeye na Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Mbeya (RCO) na wasaidizi wao wawili.

"Tulizungumza na hoja ya Kamanda Kuzaga ilikuwa kwamba, wanahitaji kumchukua Twaha Mwaipaya, kiongozi aliyekuwa anaratibu shughuli za BAVICHA kutoka Makao Makuu Dar es Salaam na Makamu Mwenyekiti wake.

"Tulimwuliza 'unawachukua unawakamata au la? Alisema anawachukua kwa lengo la kuwakamata. Tukashauriana kwa pamoja kwamba, kwa vile ndio viongozi wetu, tulimwomba atupe muda ili watueleze maandalizi ndipo aondoke nao. Alikubali na kutupa dakika 40," alidai Lissu na kueleza kuwa baadaye viongozi hao wawili walichukuliwa na polisi.

Alisema baada ya hapo giza likiwa limeingia, wakiwa wamezingirwa na polisi, Kamanda Kuzaga aliwaeleza hakuna mtu kutoka wala kuingia.

Alisema wakati wakijiandaa kwa mkesha akiwa ameahidi "kutoa shule usiku kucha juu ya mambo ya nchi", polisi waliozingira ofisi hiyo waliingia ndani na kukamata watu wakiongozwa na Kamanda Kuzaga.

"Ndipo kipigo kikaanza kwa kutumia marungu, yakiwamo ya umeme. Na mimi nikavurumishwa na 'kamguu kangu', ikawa vurumai, kilichotokea kwangu angalau, Kamanda Kuzaga alikuja akanichukua akanitoa nje akanikabidhi kwa RCO akamwambia 'mpeleke kwenye gari lako' huku nyuma nikaacha kipigo kinaendelea," alidai.

Lissu alidai kuwa akiwa katika gari, Kamishna Haji alihoji alikokuwa na kufuatwa kwenye gari la RCO na kupelekwa alikokuwa na ndipo akachukua kofia yake na miwani na kumwamuru apande gari la wazi la polisi.

"Akaniambia 'panda hilo gari', nikamwambia 'siwezi, sina mguu', akaniambia 'umekuja kutafuta nini hapa?' Kwa kuwa nilishindwa kupanda, akawaamuru wale askari wanibebe na kuniingiza katika Land Cruiser, nikasukumizwa kwenye uvungu wa viti vyao.

"Nikalala pale na baadaye walinirudishia kofia yangu na kofia ya mtu mwingine na miwani," Lissu alisimulia.

**MNYIKA**

Katibu Mkuu Mnyika alisema alikataa kutoa maelezo yake na kueleza kuwa atatoa mahakamani, akidai ndiyo sababu ya kupewa kosa la kutotii amri ya polisi kulikosababisha kuingizwa mahabusu isiyo na kitanda na alikolala hadi asubuhi kisha akasafirishwa kwa gari alilolitaja "zuri kiasi" lakini hakupewa simu zake.

"Nilipofika Kituo Kikuu cha Dar es Saalm usiku wa manani, niliwauliza askari waliokabidhiwa kwao, nimetuhumiwa kwa kosa lenye dhamana, kwanini sijapewa dhamana, sijatibiwa, sijaonana na wakili wangu wala familia?

"Waliniambia 'usiwe na wasiwasi, tunawaruhusu watu wa Njombe', baadaye waliniambia nijidhamini mwenyewe na niripoti polisi Agosti 15, 2024," alidai.

Mnyika alidai kuwa aliwaomba wamwitie usafiri wa kukodi jijini Dar es Salaam, wakamjibu watampeleka kwa usafiri wa polisi, akapelekwa hadi nyumbani kwake ambako alifika saa tisa usiku.

"Polisi walitupiga bila sababu ya kutupiga, ni kama walitumwa kufanya udhalimu kwa kuwa walikuwa wanaelewa wanachokifanya, niliona ni kaburi la 4R za Rais Samia Suluhu Hassan," alidai Mnyika.

**PAMBALU**

Mwenyekiti wa BAVICHA, Pambalu, alisema aliingia nchini Agosti 12, mwaka huu, akitokea Marekani na aliwatafuta viongozi wa chama bila mafanikio hadi alipompata Mwenyekiti Mbowe, ili wakatoe msaada wa kibinadamu na kisheria, wakisafiri kwa ndege usiku.

"Tulifika saa 5:15 usiku, wakati tunashuka Mwenyekiti hakushuka, nilivyomfikia, akaniambia 'ninaona kuna askari wengi', akauliza 'kuna mheshimiwa yoyote tunasafiri naye?', tulivyoshuka walinikamata wakanipeleka mbali na mwenyekiti, kisha tukapakizwa kwenye magari ya polisi.

"Tulipelekwa ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya. Tukiwa uwanja wa ndege, tulihoji kosa la kukamatwa, askari walijibu hawajui, bali wakubwa wao watatuambia kwanini tumekamatwa. Tulikaa kwa saa mbili, tukihojiwa, mwenyekiti hakusema chochote, mimi niliandika jina langu tu," alisema.

Nipashe ilimtafuta Msemaji wa Jeshi la Polisi Tanzania, Kamishna Msaidizi, David Misime, kwa ajili ya kupata ufafanuzi wa madai ya CHADEMA dhidi ya polisi, lakini simu yake haikupokewa.

# Adaiwa kujinyonga akiwa mahabusu ya mahakama

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

SELEMANI Mzirai (49), mkazi wa Kiluvya, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani, anadaiwa kujinyonga akiwa katika mahabusu ya mahakama wakati anasubiri kupelekwa gerezani baada ya kuhukumiwa kifungo cha maisha.

Selemani anadaiwa kujinyonga kwa kutumia shati lake alilolifunga kwenye nondo za dirisha la choo katika Mahakama ya Wilaya Kisarawe, jana.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, Selemani alihukumiwa kifungo cha maisha gerezani baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kunajisi na kulawiti mtoto wake wa kufikia mwenye umri wa miaka saba.

"Baada ya kusomewa hukumu, Selemani aliingia chooni kujinyonga kwa kutumia shati lake alilolifunga kwenye nondo za choo hicho," alidai Kamanda Lutumo.

Alisema mwili wa Selemani umehifadhiwa katika hospitali ya wilaya ukisubiri uchunguzi wa daktari na kukabidhiwa kwa ndugu kwa mazishi.

Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, inaelekeza adhabu ya kifungo cha maisha kwa anayepatikana na hatia ya kunajisi mtoto mwenye chini ya umri wa miaka 10.

Sheria hiyo katika kifungu cha 130 (1) inaelekeza, "Ni kosa kwa mtu wa jinsia ya kiume kumbaka msichana au mwanamke."

Sheria hiyo inaelekeza katika kifungu cha 130(3) kuwa, "Bila ya kujali masharti yaliyopita ya kifungu hiki mtu yeyote atakayetenda kosa la kubaka msichana wa chini ya umri wa miaka 10, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha."

Kifungu cha 131(1) cha sheria hiyo kinaelekeza, "Mtu yeyote atakayetenda kosa la kubaka, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha, na kwa kila kesi ambayo kifungo chake hakipungui miaka 30 pamoja na adhabu ya viboko na faini, na atatakiwa kulipa fidia ya kiasi ambacho kitatamkwa na mahakama, kwa mtu ambaye ametendewa kosa hilo na kwa majeraha aliyoyapata."



Ujumbe kutoka Taasisi ya Kupanda Milima ya Himalaya (HMI) chini ya Wizara ya Ulinzi ya India, ukiongozwa na Kapteni Jai Kishan (wa tatu kushoto), wakionesha bendera ya taifa ya nchi hiyo yenye ukubwa wa futi za mraba 7800 kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, waliyoipandisha katika kilele cha Mlima Kilimanjaro, baada ya kurejea hivi karibuni, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya miaka 78 ya Uhuru wa India. **PICHA: JOHN BADI**

# Janabi: Kufunga ni tiba kwa afya

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Mohamed Janabi, amesema kuwa pamoja na watu wengi kufunga kutokana na sababu mbalimbali katika jamii, kubwa ikiwa ni kutokana na imani hususan wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhan na Kwaresma, lakini ni afua ya afya.

Profesa Janabi, mwanataaluma, tabibu na bingwa aliyebobea kwenye magonjwa yaliyomo kwenye kundi la NCDs, hajutii kuwa na mlo mmoja au miwili kwa siku, akizitaja kuwa kati ya tiba ya kuondoa mabaki yasiyohitajika mwilini.

Katika kitabu chake: Mtindo wa Maisha na Afya Yako, anatoa elimu kwa umma kuhusu mbinu za kufunga na faida zake (intermittent fasting), akisema wanaofunga wanaongeza siku za kuishi; wana uzito unaowiana; wanapunguza kalori na kuokoa muda.

Prof. Janabi anazitaja faida nane za kiafya kwa mtu anayefunga, akisema ni afua muhimu katika afya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza.

"Miongoni mwa sababu za kiafya ukifunga ni kati ya hizi; Kupunguza uzito. Kufunga ni afua inayopunguza uzito na inaweza kuwa njia nzuri ya kupambana na uzito uliopitiliza. Idadi kubwa ya watu hutumia njia hii kupunguza uzito.

Ingawa kwa kundi hili ni muhimu kujiuliza kwa nini wanaongezeka uzito, ili kuzuia visababishi vitakavyowafanya kuwa na uendelevu wa kudumu, ni muhimu kujua kiini cha uzito ni nini. Watu wengi wanashindwa kutambua hasa nini chanzo cha kuongezeka uzito."

Anasema pamoja na kufunga kuwa sababu ya kupungua uzito, ni vyema anayehitaji kupungua uzito kuzingatia sababu za kuongezeka kwa uzito.

Anaitaja faida ya pili ya kufunga kuwa ni; Ukinzani wa wingi wa insulini mwilini (Insulin Resistance).

"Ili kuweza kutumika kwa ajili ya kuupa mwili nguvu, chakula humeng'enywa na ili kufanywa kuwa katika chembechembe rahisi kuchakatwa ili kuzalisha nguvu na viini lishe kuujenga mwili.

Vyakula vyenye asili ya wanga (carbon hydrates) au sukari na kwa uchache sana protini, kikishaingia mwilini, kiungo cha mwili kinachoitwa kongosho (pancreas) hutoa kichocheo cha insulini.

Kongosho, ni kiungo maalumu ambacho kazi yake ni kuzalisha insulini. Insulini inafanya kazi ya kuchukua sukari au wanga uliozidi na kuhifadhi kama mafuta. Kwa kawaida sukari na wanga huhifadhiwa katika sehemnu mbalimbali mwilini kama vile kwenye ini, misuli au tumbo (kitambi).

Ikiwa mwili utapokea kiasi kikubwa cha wanga na mafuta zaidi ya kinachohitajika, kinaongeza mzigo mkubwa kwa kongosho katika uzalishajl wa insulini."

Anasema mzigo mkubwa kwa kongosho matokeo yake ni kusababisha kushindwa kwa insulini kuhimili kazi yake na sukari au mafuta vinabaki katika mifumo yake katika mishipa ya damu na hali hiyo ya uzalishaji wa insulini nyingi isiyofanya kazi kama inavyotakiwa, husababisha kutokea kwa ukinzani wa insulin.

Hali hii inaweza kuwa ndio hatua ya kuingia kwenye matatizo ya kisukari ambayo ina aina pili ambayo hutokana na maadiliko ya mwili, mfumo na ulaji. Tofauti na aina ya kisukari cha kuzaliwa nacho."

"Takwimu za kitabibu zinaonyesha kuwa watu tisa kati ya 10, wana ukinzani wa insulini bila ya kujitambua. Kitaalamu, mwili unapokuwa na ukinzani wa insulini uzito wa mwili unaongezeka.

Jambo hili ni muhimu kwa kuwa ndio moja ya sababu kubwa ya kuongezeka uzito wa mwili.

Watu wenye kisukari aina ya pili (Type II Diabetes) wanaotumia vidonge uzito wao upo juu kwa sababu insulini ipo juu mwilini mwao.

Moja ya kazi kubwa ya insulini mwilini ni kutunza chakula (kuweka akiba) katika mfumo wa mafuta. Kwa maana hiyo, insulini inageuza sukari na wanga kuwa mafuta na kuhifadhi mwilini hali inayosababisha ongezeko la uzito.

Kwa maana hiyo basi, tunaweza kusema uzito ni matokeo ya ukinzani wa insulini."

Bingwa huyo wa Magonjwa ya Moyo mwenye shahada tatu katika sayansi ya tiba, anasema kufunga ni mbinu ya kukiepuka kisukari.

Sukari ikiwa sawa inaweza kusababisha mabadiliko ya matibabu wanayopata, kupungua kwa vidonge, sindano na dozi wanazopata au hata kusimamishwa kutumia dawa kabisa na kutumia chakula kama tiba.

Kisukari (Diabetes Mellitus Type 2) ni ugonjwa wa lishe na tiba yake kuu lazima iwe lishe. Hali hii huwapa unafuu kutokana na madhila ya kisukari. Afua hii ikitumika vyema na kwa uangalifu, inaweza kupunguza tatizo kubwa la sukari.

Kwa wale waliopo katika hatua za awali za kisukari (prediabetes), afua hii inaweza kuongeza muda mrefu kabla ya mtu kuwa mgonjwa kamili. Lakini inaweza kuipa kongosho afueni na hivyo kurejesha afya na kuwa nzima.

Upo ushahidi wa kisayansi unaoonyesha kuponywa kwa watu wanaoishi na kisukari, au waliopo katika hatua za awali kupona kwa kuzingatia afua hii kwa uangalifu na ufuatiliaji wa karibu wa afua hii na afua nyingine."

**TAKWIMU ZA NCDs**

Takribani vifo nusu milioni ambavyo vingeepukika, hutokea kila mwaka. Shirikia la Afya Duniani (WHO), linasema.

Nchini MagonjwaYasiyoambukizwa (NCDs), huchangia takribani asilimia 70 ya magonjwa mengine kama vile figo na moyo. Asilimia tisa ya Watanzania wanaugua kisukari huku asilimia 15 wakiugua presha, kwa mujibu wa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

## Wapanda mlima Himalaya waja kupanda Kilimanjaro

**Na Romana Mallya**

UJUMBE kutoka Taasisi ya Wapanda Milima ya Himalaya (HMI), inayofanya kazi chini ya Wizara ya Ulinzi India, umefika nchini na kupanda Mlima Kilimanjaro kupeleka ujumbe duniani kuwa wenye ulemavu wakiwezeshwa wanaweza kufanya mambo makubwa.

Kiongozi wa msafara huo kutoka Hifadhi ya Kanchenjunga, India unaoongozwa na Jai Kishan, ameambatana na watu wengine watano miongoni mwao yuko mwenye ulemavu wa mguu, Uday Kumar na wengine ni Sulaxchana Tamang, Kampteni Shruti, Mahendra Yadav na Pawel Sharma.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam na waandishi wa habari katika Ubalozi wa India Nchini, Kishan alisema baada ya kuanza safari ya kupanda mlima huo, Agosti 7, mwaka huu, walifika kituo cha Kibo.

"Agosti 8, mwaka huu, tulifika kilele cha Uhuru, tukiwa tumesimama kwenye mwinuko wa mita 5,895 (futi 19,341), tulionesha dunia bendera yetu ya India yenye ukubwa wa futi za mraba 7,800," alisema.

Alisema wamepanda mlima huo pia, kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 78 ya Uhuru wa India na kujivunia mafanikio yaliyofikiwa katika nyanja mbalimbali.

Kadhalika, alisema wameonesha dunia kuwa wenye ulemavu wanaweza kufanya mambo makubwa zaidi, huku wakitoa wito kwa taasisi zinazojihusisha na kundi hilo kuwasaidia kutimiza ndoto zao.

"Baada ya kupanda Mlima Kilimanjaro ushauri wetu kwa ujumla, ni serikali kuangalia uwezekano wa kutengeneza njia zenye urahisi kwa wenye ulemavu, ili kuwezesha kupanda mlima huo kwa urahisi," alisema.

Pia, alisema wanaionesha dunia kuwa wenye ulemavu wanaweza kushinda vikwazo na kufanikisha mambo makubwa.

Alihamasisha jamii kutoa matumaini kwao kwa sababu ulemavu haupaswi kuwa kikwazo cha kufikia malengo makubwa maishani.

Kumar ambaye anawakilisha kundi la wenye ulemavu, alisema ameshiriki upandaji Mlima Kilimanjaro kuonesha na kuelezea ulimwengu kwamba hakuna kisichowezekana.

"Ujumbe wangu kwa watu wenye ulemavu duniani waje Tanzania kwa utalii," alisema.

# Ugonjwa afya ya akili watesa kinamama baada ya kujifungua

Na Jenifer Gilla

USTAWI wa afya ya akili ya mama wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua ni suala muhimu, lakini utafiti umebaini halipewi kipaumbele nchini.

Imebainika kuwa, kutokana na suala hilo kutopewa kipaumbele, kinamama wengi wanakosa msaada, hivyo kupata madhara yanayotajwa kuchangia ongezeko la wagonjwa wa akili nchini.

Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kliniki Kilimanjaro mwaka 2018 kwa wanawake 1,128 wilayani Moshi, ulibaini kwamba, mmoja kati ya 10 (asilimia 12.2) alikuwa na changamoto ya afya ya akili ya baada ya kujifungua.

Utafiti mwingine uliofanywa na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) mwaka 2015 kwa wajawazito 1,180, ulibaini kwamba, wanane kati ya 10 (asilimia 78.2) walikuwa na shinikizo la damu na dalili za wasiwasi wakati wa ujauzito.

Hospitali hiyo ya ngazi ya juu zaidi kitaifa, pia ilibaini kuwa asilimia 49 ya kinamama hao 1,180 waliokuwa na ujauzito, walikuwa na dalili za mfadhaiko.

Maria Gregory (40), mkazi wa Mbezi, wilayani Ubungo, mkoani Dar es Salaam, anasimulia alivyochoshwa na vilio visivyokoma vya mtoto wake mchanga, hata kufikiria kujiua.

"Mtoto alikuwa analia usiku kucha, mume wangu akahama chumbani na kuniachia mzigo wa kubembeleza mtoto huku ninauguza kidonda, maana nilijifungua kwa upasuaji.

"Kutokana na uchovu niliokuwa ninapata kutokana na misukosuko ya malezi na kelele hizo za mtoto, nikapata hisia za kumchukia mwanangu. Usiku nilikuwa ninachoka na kuhisi kuchanganyikiwa.


"Mtoto anataka umbebe tu, ukimlaza analia, sikuwa na msaada na nilijikuta mtoto anapolia, ninalia naye na kuna wakati nilipata mawazo ya kujiua.

"Hata nilipomshirikisha mama yangu mzazi kuhusu madhila haya, alinishauri niende kanisani kuombewa kwa kuwa aliona ajabu 'mama kuchukia mtoto wake mchanga', akahisi nimepatwa na mapepo," Maria anasimulia.

Mama huyo wa watoto watatu mwenye shahada ya ualimu, anasema kuwa na msongo huo wa mawazo kwa miezi mitatu, alipokwenda kliniki, alimweleza muuguzi kuhusu hali yake; naye akashauri apumzike kwa muda mrefu, jambo ambalo lisingewezekana kwa kuwa hakuwa na mtu wa kumsaidia kazi za nyumbani.

"Nilipata hofu kwamba ningekufa na kuacha watoto wangu wakiteseka. Nikaperuzi mtandaoni kuhusu ile hali na namna ya kukabiliana nayo. Nilipanga ratiba ya kupumzika wakati wa mchana mama alipokuja kunisalimia.

"Baadaye nikaajiri yaya wa kusaidiana naye kulea mtoto usiku, na nikatafuta msaada wa kiroho kutoka kwa wachungaji, miezi sita baadaye nilipona kabisa," Maria anasema.



Tatu Athumani ni mama wa watoto watatu kama ilivyo kwa Maria, tofauti yao yeye ni mkazi wa Tabata jijini Dar es Salaam na ni mdogo kwa miaka miwili kwa maana ana umri wa miaka 38.

Anasema kuwa, baada ya kujifungua mtoto wake wa tatu (wa kike), alijikuta akielemewa na kazi za nyumbani huku akiwa na mtoto mwingine mdogo mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu.

**"Hata nilipomshirikisha mama yangu mzazi kuhusu madhila haya, alinishauri niende kanisani kuombewa kwa kuwa aliona ajabu 'mama kuchukia mtoto wake mchanga',**

"Sikutaka kuhudumiwa na mtu yeyote. Hapo nilikuwa na watoto wengine wawili; mkubwa alikuwa na umri wa miaka minne na alihitaji kuandaliwa kila siku kwa ajili ya kwenda chekechekea (shule ya awali).

"Nilijikuta nina uchovu sana na hasira mara kwa mara. Wakati mwingine nilijifungia chumbani na kulia kutokana na kuhisi upweke hadi mume wangu aliporejea nyumbani jioni na kunisaidia baadhi ya kazi.

"Msaada wa mume wangu haukuwa mkubwa kwa sababu alikuwa anashinda kazini muda mwingi, alikuwa anarejea nyumbani saa 10 jioni na kuondoka alfajiri.

"Nilidumu katika hali hiyo kwa takribani miezi minane nisijue la kufanya, marafiki zangu wakanishauri kuvumilia kwa maelezo kuwa hata wao walipitia hali hiyo na ikaisha. Baadaye nilipata akili ya kuleta msaidizi, nikapata nafuu," Tatu anasema.

Farhat Rashid, mkazi wa Unguja, anasema alipata msongo wa mawazo wakati baada ya mumewe kumwacha na kuoa mke mwingine wakati akiwa na ujauzito wa miezi sita.

"Nilipopata taarifa ameoa, nikawa na mawazo na maswali mengi yasiyo na majibu, muda mwingi nilijifungia chumbani peke yangu na kulia, hadi pale mama alipomweleza daktari wakati wa kliniki, akanitafutia mtaalamu wa saikolojia, akanisaidia kukubaliana na hali ya kuachwa, nikapata nafuu," anasema Farhat.

Daktari wa Magonjwa ya Wanawake MNH, Benny Kimaro anasema anakutana na kesi tatu hadi nne kila mwezi za wanawake wanaopata changamoto ya afya ya akili baada ya kujifungua.

Dk. Kimaro anasema ugonjwa huo huathiri kinamama baada ya kujifungua na dalili hutokea kati ya siku ya tatu hadi tano baada ya kujifungua.

"Mama anapitia hisia hasi kama vile upweke, kulia mara kwa mara, kutopenda mtoto wake. Kama akichelewa kupata matibabu, anaweza kumdhuru hata mwanae.

"Ni hali inayosababishwa na mambo mbalimbali, ikiwamo mabadiliko ya homoni wakati wa ujauzito, ujauzito usiotarajiwa, changamoto za kiafya kama vile shinikizo la damu na ukosefu wa msaada wakati wa miezi ya mapema ya utunzaji mtoto," Dk. Kimaro anasema.

Kukabaliana na maradhi hayo, Dk. Kimaro anashauri wanaume washiriki kikamilifu kulea watoto katika miezi ya mwazo ya mtoto na kutowanyanyapaa wenza wao pale wanaoonesha dalili za afya ya akili, bali wawapeleke kituo cha afya.

Msaikolojia Tiba kutoka Kituo cha Afya Somedics, jijini Dar es Salaam, Dk. Saldin Kimangale anasema wanawake wanaopata tatizo hilo, hukosa furaha, usingizi, hamu ya kula, na kuwa mtazamo hasi kuhusu wao wenyewe, hasira na msongo wa mawazo.

Dk. Kimangale anashauri wanawake kujiepusha na mimba zisizotarajiwa na elimu itolewe katika kliniki za wajawazito ili watambue na kujiepusha na visababishi vya ugonjwa huo pamoja na kuhakikisha wanapata msaada wa kutosha baada ya kujifungua.

"Mgonjwa wa afya ya akili anapopeletwa katika kituo chetu cha afya huwa tunamtibu kulingana na ukubwa wa tatizo; kuna wanaohitaji ushauri nasaha, wengine vidonge na wale walioathirika zaidi hulazwa katika vituo maalum, ikiwamo kupelekwa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Milembe," anasema.

Dk. Luzango Maembe, Mtaalamu wa Magonjwa ya Wanawake katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala, Dar es Salaam, anathibitisha hospitali hiyo kupokea wagonjwa wanawake wenye changamoto za afya ya akili, wengi wakifikishwa hospitalini huko ugonjwa ukiwa umefika katika hatua ya mwisho ya kuhitaji kulazwa.

Anashauri jamii ipewe elimu ya mara kwa mara ili ione ugonjwa huo kama magonjwa mengine na mgonjwa apelekwe kituo cha afya pale tu anapoonesha dalili za mwanzo badala ya kusubiri mpaka aathirike zaidi.

Kwa Tanzania, mtumishi mwanamke akijifungua anapewa siku 84 za likizo ya uzazi kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini huku mumewe akipewa siku tatu za kusaidia malezi ya mtoto aliyezaliwa.

Shabani Mwinyiheri, mkazi wa Temeke, Dar es Salaam, anashauri sheria hiyo ifanyiwe maboresho ili kumwongezea baba muda wa kukaa nyumbani kumsaidia mama kulea angalau kwa mwezi mmoja.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akiwasilisha bungeni Mei mwaka huu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2024/25, alisema kwamba, hadi kufikia Julai 2023, kulikuwa na wagonjwa 293,952 waliohudhuria katika vituo vya kutolea huduma za maradhi ya afya ya akili Tanzania Bara.

Pasi na kutaja idadi halisi ya kinamama waliokumbwa na maradhi ya afya ya akili baada ya kujifungua, Waziri Ummy alisema wagonjwa afya ya akili 19,506 waliripotiwa kulazwa hospitalini mwaka 2023/24 kulinganisha na wagonjwa 13,262 waliolazwa mwaka wa 2022/23.

Alisema takwimu hizo zinaonesha kuwapo kwa ongezeko la uelewa wa jamii kuhusu suala hilo na kuwapo vituo vya afya vinavyotoa matibabu kwa kundi hilo.

## NGO zapinga kifungu sheria kupambana rushwa ya ngono

**Na Mary Geofrey**

WANAMTANDAO wa kupinga rushwa ya ngono Tanzania, wanapendekeza kufutwa kifungu cha 10(b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Ngono, kwa kuwa kinahalalisha kuendeleza matumizi mabaya ya mamlaka kwa njia ya kumhukumu mwathirika kama mbinu ya kuwanyamazisha na kuzima mapambano hayo.

Badala yake wamependekeza kubaki kifungu cha 25 kama kilivyo kwasababu kinajitosheleza bila kumbagua mhalifu awe wa kike au wa kiume.

Tamko hilo lilisomwa jana na Mwanaharakati wa Mtandao huo, Mary Ndalo, kwa niaba ya wanamtandao hao na washiriki wote wanaopigania haki za binadamu na makundi ya pembezoni, kutoka takribani asasi 200 kuanzia ngazi ya jamii hadi Taifa.

Ndalo alisema mapendekezo yao yalikuwa ni kufutwa kifungu cha nyongeza cha 25 (b) kilichompokonya mhanga haki na badala yake kuongeza kifungu cha 10 (b), kinachohalalisha kuendeleza matumizi mabaya ya kuzima mamlaka kwa njia ya kumhukumu mhanga wa rushwa ya ngono.

"Sisi wanamtandao tunapinga rushwa ya ngono, tunatambua nyongeza ya kifungu cha 10 (b) ni kinyume kabisa na sheria ya Kimataifa, Sheria za Kuzuia Rushwa za SADC, Umoja wa Afrika na kanuni zote zinazoongoza Muungano wa Afrika Mashariki zinazokataza rushwa ya ngono," alisema.

Mwanamtandao, Avemaria Semakafu, alisema wanadai Bunge ambalo linawakilisha wananchi kutopitisha mabadiliko hayo kwa sababu kazi yake ni kutunga sheria za kulinda haki, sio kutunga sheria ya kumlinda mhalifu.

"Na tunatoa wito kwa Watanzania wote, watetezi wa haki za binadamu, hususani za wanawake na watoto wa kike kupinga vikali kuingizwa kwa kifungu cha 10 (b) kwenye huu mswada," alisisitiza Avemaria.

Mwanamtandao, Hilda Stiwati, alisema endapo bunge litapuuza madai yao, wanatoa wito kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kukataa kuridhia mabadiliko yanayowasilishwa bungeni kwa kuwa athari zake ni kubwa kwa Taifa.

Mtando huo pia ulihusika na uchambuzi yakinifu wa mapendekezo ya awali ya marekebisho ya sheria hiyo na kutoa tamko lao kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

# LATRA yatangaza ukomo kwa wahudumu mabasi wasiosajiliwa

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imesema mwisho wa kutumia wahudumu wa mabasi ya masafa marefu yaendayo mikoani na nchi jirani ambao hawajasajiliwa ni Desemba, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA, Salum Pazzy, alisema Januari Mosi, mwakani, hawatoruhusu watoa huduma ya usafiri wa masafa marefu kutumia wahudumu ambao hawajasajiliwa.

"Kanuni ya 17 ya uthibitishaji wa madereva na usajili wahudumu wa magari ya kibiashara za LATRA, mwaka 2020 zinamtaka mtu yeyote anayekusudia kufanya kazi ya uhudumu katika gari linalotoa huduma za usafiri kibiashara, kusajiliwa na mamlaka hiyo," alisema Pazzy.

"Maana yake ni kwamba tunapofika Januari Mosi, mwaka kesho, hatutowaruhusu watoa huduma kutumia wahudumu ambao hawajasajiliwa kama tulivyoeleza kwa mujibu wa sheria, hivyo tunawakumbusha wahudumu wote ambao wamepata mafunzo, kutuma maombi ya usajili." Alisema zipo faida mbalimbali za kusajili wahudumu kwenye mabasi hayo, ikiwamo kurasimisha fani na ajira ya uhudumu kwenye vyombo hivyo vya moto, kuongeza uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa mujibu wa sheria na kujenga ari ya umoja na mshikamano miongoni mwa wahudumu hao.

> **"Kanuni ya 17 ya uthibitishaji wa madereva na usajili wahudumu wa magari ya kibiashara za LATRA, mwaka 2020 zinamtaka mtu yeyote anayekusudia kufanya kazi ya uhudumu ...**

Alitoa rai kwa watoa huduma za mabasi hayo ya masafa marefu na nchi jirani kuwahimiza watoa huduma wao kwenda kupata mafunzo kwenye Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), na baada ya mafunzo wanatakiwa kuwasilisha maombi ya kusajiliwa LATRA kwa ajili ya kupatiwa kadi maalumu ya usajili wa mhudumu wa mabasi ya abiria.

"Na mamlaka kwa sasa imeendelea kusajili wahudumu hao ambao wamepata mafunzo hayo katika vyuo mbalimbali nchi nzima. Kadhalika, alisema mamlaka hiyo imeandaa tuzo maalumu kwa watoa huduma bora na salama za mabasi ya mikoani na nchi jirani.

Aidha, alisema wameamua kuanzisha utaratibu huo wa utoaji tuzo, ili kuwachochea watoa huduma hao kutoa huduma nzuri, bora na salama.

Kaimu Naibu Mkuu wa Chuo CBE, Dk. Nasibu Mramba, alisema miongoni mwa wanayoyafundisha kwa wahudumu hao wa mabasi ni sheria, kanuni na maadili zinazohusiana na usafirishaji abiria, usalama na uokoaji endapo kunatokea tatizo lolote wakati safari.

Pia alisema wanawafundisha afya pamoja na mazingira hususani inapotokea abiria anaugua au kunatokea tatizo lolote wakati wa safari pamoja na weledi wawapo kazini.

"Na mafunzo yetu huwa yanakwenda kwa siku saba na yanafanyika kwa vitendo na baada ya hapo, wanafunzi hufanya mtihani na wanaofaulu wanapewa vyeti ambavyo wanavipeleka LATRA kusajiliwa rasmi," alisema Mramba.

Mratibu wa mafunzo ya watoa huduma kwenye vyombo vya moto wa Chuo cha NIT, Honesta Msaki, alisema mpaka sasa wameshatoa mafunzo kwa watoa huduma zaidi ya 500 katika kanda mbalimbali.




Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Kiislam Tanzania (JUWAKITA), Shamim Khan (kushoto), akizungumza wakati wa kongamano la biashara la Halal, lililoandaliwa na MICO Halal International Bureau, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# NBC yajitosa kuinua uzalishaji kahawa

**Na Mwandishi Wetu,** MBINGA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imetambulisha rasmi kampeni yake ya 'Shinda Mechi Zako Kinamna Yako na NBC Shambani' wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma, ikilenga kuchochea kasi ya uzalishaji kahawa wilayani humo kupitia huduma zake mahsusi na zenye upendeleo kwa wakulima wa zao hilo.

Imetambulishwa kwa mara ya kwanza kampeni hiyo inayokwenda sambamba na mafunzo ya huduma mbalimbali zinazotolewa na benki hiyo, ikiwamo huduma ya bima ya mazao na bima za afya, uwakala, huduma za kidigitali, mikopo ya zana za kilimo na pembejeo.

Huduma nyingine ni pamoja ujenzi wa maghala na kusaidia wakulima shughuli mbalimbali zinazohusiana na maandalizi ya msimu wa kilimo na masoko ya mazao yao.

Hafla ya utambulisho wa huduma hiyo ilifanyika jana wilayani Mbinga, ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Kisare Makori, ikihudhuriwa na viongozi wengine waandamizi wa mkoa huo pamoja na wadau mbalimbali wa zao hilo, wakiwamo viongozi wa vyama vya ushirika na wakulima.

Mkuu wa Kitengo cha Mikakati wa NBC, Msafiri Shayo, aliwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Theobald Sabi kwenye tukio hilo.

Akizungumzia hatua ya benki hiyo, Makori pamoja na kupongeza benki hiyo kwa kutoa kipaumbele kwa wakulima nchini kupitia huduma zake, alisema ujio wa kampeni hiyo wilayani mwake ni ukombozi kwa wakulima wa kahawa wanaohitaji upendeleo maalum wa huduma za kifedha. Serikali imejipanga kuhakikisha dhamira ya benki hiyo inafanikiwa.

"Zaidi nimefurahi kusikia kwamba kupitia kampeni hii wakulima wanaweza kupata mikopo ya vitendea kazi muhimu kama vile matrekta na zana nyingine za kisasa za kilimo, pembejeo za kilimo na mikopo ya malipo ya awali kwa wakulima.

"Pia huduma za bima za afya na kilimo zinazohamasishwa na NBC kupitia kampeni hii ni muhimu sana kwa wakulima, hasa katika kukabiliana na changamoto za kiafya kwa wao binafsi na familia zao na kujilinda dhidi ya hasara zitokanazo na majanga ya asili ambayo yanaweza kuathiri mazao yao," alisema.

Makori pia alieleza kuvutiwa na kuwapo kwa zawadi zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 30 zitakazotolewa kwa wakulima watakaoshinda droo mbalimbali baada ya kufungua akaunti ya NBC Shambani na kuweka fedha zao za mauzo ya kahawa.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Msafiri alisema kampeni hiyo ni sehemu ya mwitikio wa benki hiyo kufuatia wito wa serikali wa kuchangia katika kufanikisha agenda 10/30 inayolenga kuongeza uzalishaji mazao ya kilimo kutoka asilimia tano hadi 10 ifikapo mwaka 2030.

Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo, Lariba na Wakulima NBC, Raymond Urassa, alisema kampeni hiyo inalenga wakulima wote wakiwamo mmoja mmoja, vyama vya ushirika na vyama vya msingi vya mazao ambao watapitisha fedha za mauzo katika akaunti zao za NBC Shambani.

Akizungumza kwa niaba wakulima hao, Loveness Kapinga, Katibu wa AMCOS ya Nahongo wilayani hapa, alionesha kuvutiwa na huduma za bima za afya na bima za kilimo kutokana na hitaji kubwa walilonalo wakulima hao katika upatikanaji huduma za afya.

Hiyo ni mara ya kwanza kwa kampeni ya NBC Shambani kuingia mkoani Ruvuma, ikiwa tayari ina misimu mitatu katika mikoa mingine, ikiwamo Mtwara na Lindi ambako benki hiyo imeweka kipaumbele kuinua uchumi wa wakulima na vyama vya ushirika vya mazao ya korosho, mbaazi na ufuta.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ulaji sahihi unavyopunguza hatari ya magonjwa yasiyoambukiza

**MAGONJWA** yasiyoambukiza yanaelezwa kusumbua watu wengi hasa wenye umri mkubwa kutokana na kutozingatia vizuri mtindo wa maisha yao.

Magonjwa yasiyoambukiza ni yale ambayo hayasambazwi kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kwa kuwa hayana vimelea vinavyohusiana na magonjwa hayo.

Katika nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwa mojawapo ajali za barabarani na madhara yatokanayo na vilevi yamewekwa kwenye orodha ya magonjwa yasiyoambukizwa.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), magonjwa yasiyoambukiza ndio yanayoongoza kwa kusababisha vifo duniani.

Utafiti unasema asilimia 72.8 duniani ya vifo vinasababishwa na magonjwa yasiyoambukiza na shinikizo la damu limekuwa kichocheo kikubwa.

Utafiti huo uliofanywa na Nature mwaka 2007 umeripoti kuwa magonjwa yasiyoambukiza yanaua kwa kasi zaidi kulinganisha na yale yanayoambukiza.

Kutokana na takwimu hizo za kidunia kwa hapa nchini katika utafiti uliofanywa mwaka 2012, unaonesha kuwa asilimia 92.6 ya Watanzania ambao vipimo vyao vya shinikizo la damu vina walakini, hawajaanza kutumia dawa, hali inayowafanya kuwa katika hatari ya kupata magonjwa mengine yasiyoambukiza.

Ulaji chakula bila kuzingatia kanuni za afya umeelezwa kuwa chanzo kinachochangia magonjwa hayo kuwakumba watu wengi.

Hivi sasa hospitali nyingi zinapokea wagonjwa wenye magonjwa yanayotokana na tatizo la shinikizo la damu, moyo, figo na mengine ambayo chanzo chake ni mtindo wa maisha wanayoishi.

Wataalamu wa afya mara kwa mara wanashauri watu kuzingatia ulaji uliosahihi na kufanya mazoezi ili kujikinga na maradhi hayo.

Kwa mujibu wa wataalamu hao magonjwa yasiyoambukiza yanatumia gharama kubwa katika matibabu ya wagonjwa kulinganisha na magonjwa mengine.

Magonjwa hayo yanaweza kudhibitiwa kwa watu kufuata kanuni za afya ikiwamo pia kucheki afya zao mara kwa mara ili kujua mwenendo wao.

Kuna wakati mtu anakwenda hospitali kutibiwa tatizo lingine, lakini anapofika na kuangaliwa mwili wake anakutwa na tatizo kubwa. Utafiti unaeleza kuwa umri wa kuishi kwa wanawake ni miaka 69 na wanaume umepungua kwa sasa wanaishi miaka 62 kwa ajili ya changamoto mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabianchi, mazingira na mabadiliko katika maendeleo.

Magonjwa yasiyoambukiza imeelezwa kuwa ni changamoto hasa katika umri wa wazee na kila mara kumekuwa kukitolewa elimu kwa kuwashirikisha watu wenye umri huo kuwakumbusha kufanya mazoezi ya viungo ambayo yanasaidia kutoa sumu mwilini na kuimarisha mifupa na nyonga.

Moja ya mambo yanayochangia kuongezeka kwa magonjwa hayo ni mabadiliko ya taratibu za kimaisha zinazohusisha matendo yanayoweza kusababisha magonjwa.


Moja wapo ni kukaa muda mrefu sehemu moja kama vile ofisini au darasani na kutojihusisha katika shughuli za michezo.

Ulaji usiofaa. Kula chakula kuzidi mahitaji ya mwili, kula chumvi na sukari kuliko mahitaji ya mwili ni vitu vinavyochangia kuongezeka kwa magonjwa hayo.

Dalili za magonjwa yasiyoambukiza ni watu kujiona kuchoka bila sababu, kichwa kuuma mara kwa mara, macho kutoona vizuri, kushikwa na kizunguzungu mara kwa mara, kutokwa na damu kwenye fizi mara kwa mara, miguu na mikono kuwa na maumivu kama ya kuwaka moto na nyingi zinazofanana na hizo.

Mtu akishaona dalili hizo ni bora akimbilie hospitali na kubadili mtindo wake wa maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Dira 2050 ihimize kilimo kinachopunguza kemikali

**DUNIA** ya sasa na Tanzania yetu maradhi hasa yasiyoambukiza kama saratani na changamoto za ini ni mengi na vyanzo vyake vinatajwa.

Licha ya watu kuelezwa kuwa maisha ya kubweteka na ulaji usio na mpangilio unaojaa wanga zaidi kuliko mlo kamili ni tatizo, upande mwingine sumu na kemikali kwenye vyakula zina mchango.

Ulaji wa nafaka zinazohifadhiwa na kutunzwa kwa kemikali za sumu waweza kuwa mwanzo, lakini pia kunyunyizia dawa hizo kwenye mboga na matunda mashambani na bustani vinahusika pia.

Kemikali hizo zinachafua vyakula , maji na ardhi na kuathiri mazingira na ikolojia nzima.

Ni kweli kuna wadudu vamizi waliotokea sehemu mbalimbali duniani kuanzia Amerika hadi Afrika, wanaoshambulia mazao.

Wanaharibu uzalishaji wa mazao ya chakula hadi ya biashara na wamesambaa kila mkoa, na ili kulima na kuvuna kwa tija ni lazima kuwatibu kwa kemikali za sumu.

Wadudu hawa wana athari kubwa wanashambualia mazao hatua zote kuanzia mbegu ,miche, majani, shina, maua na matunda.

Wanakula mboga, nafaka, matunda ya mazao jamii ya nyanya ikiwamo nyanya chungu, hoho mnavu, pilipili aina zote, ngongwe, biringanya na magugu yenye jamii ya nyanya kama ndulele hivyo kusambaa kwa haraka.

Lakini, ni lazima kutafuta dawa. Inapoandaliwa Dira ya Taifa 2050 ni lazima kuweka mkazo wa kuwa na chakula salama.

Mpango uende na kuwa na wataalamu pamoja na na viwanda vya kukizalisha viuatilifu hai vya kupambana na wadudu hao ili kulihakikishia taifa usalama na ulinzi wa chakula.

Ni vyema sasa kuwa na taasisi za kuchochea uzalishaji huo kwa ngazi zote kuanzia vijijini hadi mijini na pia kuwa na maabara kubwa kwa usajili na uchunguzi na kujenga viwanda na uwekezaji mkubwa kwa kushirikisha wawekezaji wenye nia ya kuleta usalama kwenye chakula na kulinda mazingira.

Ni lazima pia kuwaeleza wananchi kutumia dawa za asili ili kuua visumbufu, kurutubisha mimea, kupunguza matumizi ya mbolea za kemikali na kulinda wadudu rafiki kama nyuki ili kuongeza uchavushaji na mavuno.

Mahindi ni zao kuu la chakula likilimwa karibu mikoa yote kuanzia Shinyanga, Kilimanjaro, Tanga, Mwanza, Arusha, Morogoro, Tabora, Pwani, Dar es Salaam, Iringa, Njombe, Mbeya na Manyara.

Lakini kote huko linashambuliwa na visumbufu na kutishia hatma ya zao hilo na upatikanaji wa chakula.

Ni vyema pia Dira ya 2050 iangazie uzalishaji wa viuatilifu hai na mbolea za asili ili kuleta afya na usalama wa chakula na kupunguza matumizi ya kemikali ambazo zinaweza kuathiri bayoanuai na kuua Watanzania.

Ikumbukwe kilimo kina umuhimu wa kipekee kwenye kufikia utoshelevu na usalama wa chakula ni lazima Dira ya 2050 ilete mabadiliko ya kufikia kilimo hai na kuongeza tija katika uchumi endelevu kwa Watanzania.

Ni lazima kuwa na viuatilifu na mbolea hai zisizo na kemikali wala viambata sumu lakini vinavyoua wadudu na kuboresha udongo na mimea pamoja na kuondoa usugu kwa wadudu kwa, mfano zama hizi mahindi yanaposhambuliwa na wadudu unaweza kutumia dawa mara nyingi lakini ghafla wanaibuka tena.

Ni kutokana na usugu hivyo, mkazo uwekwe kwenye viuatilifu asilia ili kuondoa usugu huo ambao unaathiri ikolojia na maisha ya viumbe na wanadamu.

Ikumbukwe wadudu wengi wamekuwa sugu kwenye viuatilifu vya kemikali ambazo ni hatari kwani zinaacha mabaki ya sumu kwenye mazao na ardhini.

Ni lazima pia dira isimamie na kuendeleza uhifadhi wa bayoanuai na teknolojia zinazotunza mazingira kwa uendelevu ambazo ni za asili.

HABARI KITAIFA

# Majaliwa, Makamu wa Rais Cuba wateta

**HAVANA,** CUBA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Serikali za Tanzania na Cuba zitaendelea kushirikiana katika sekta za elimu, afya, kilimo, utalii na masuala ya teknolojia.

Ameeleza hayo baada ya mazungumzo yake na Makamu wa Rais wa Cuba, Salvador Valdes Mesa yaliyofanyika Revolutionary Square, jijini Havana, Cuba.

Majaliwa ambaye yuko Cuba kwa ziara maalum ya siku mbili kwa ajili ya kuboresha uhusiano baina ya Tanzania Cuba, alisema kuwa Wizara za Elimu za Tanzania na Cuba zinaendelea kutekeleza makubaliano ya muda mrefu ambapo Watanzania wengi wamesoma na wanaendelea kusomea udaktari Cuba.

Alieleza kuwa Wizara ya Afya ya Tanzania imekuwa ikialika madaktari bingwa kutoka Cuba kwenda Tanzania kushirikiana na madaktari wa kitanzania kutoa huduma ya matibabu ya kibingwa kwa watanzania katika maeneo mbalimbali nchini.

"Tumeshuhudia mara kadhaa madaktari kutoka Cuba wakija Tanzania kufanya kazi katika hospitali kama vile Muhimbili - Upanga, Mloganzila, Bugando, KCMC na Dodoma na wakati wote wamefanya kazi zao kwa bidii na uzalendo.

"Nimemhakikishia Mheshimiwa Makamu wa Rais kuwa tuendelee kuenzi ushirikiano huo wa kidugu," Majaliwa alisema.

Kuhusu sekta ya utalii, Waziri Mkuu alisema Tanzania inayo mengi ya kujifunza kutoka Cuba kwa kuwa nchi hiyo imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kukuza utalii wa fukwe baada ya kuwa imejenga hoteli za kitalii, miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na kuwa na utaratibu mzuri wa magari ya kubeba watalii.

"Wananchi wa Cuba wanapokea watalii wengi sana, upo umuhimu mkubwa kwetu kujifunza mbinu wanazotumia kuvutia watalii wengi kutoka sehemu mbalimbali duniani," alisema.

Vilevile, katika kikao hicho, waligusia suala la kukuza Kiswahili, Ubalozi wa Tanzania Cuba ukiongozwa na Balozi Humphrey Polepole ukijitwika jukumu la kusimamia mchakato mzima wa kufundisha na kufanya lugha hiyo izungumzwe na kusambaa Cuba na katika nchi za Latin Amerika.

"Hivi sasa Kiswahili kinafundishwa katika Vyuo Vikuu vya Cuba na wanachuo wengi wanajitokeza kujifunza," alisema Majaliwa.

Balozi wa Tanzania Cuba, Polepole, alisema ziara ya Waziri Mkuu nchini humo imekusudia kukuza uhusiano wa kisiasa, kiuchumi, kibayoteknolojia na katika maeneo ya taaluma kwa faida ya nchi mbili hizo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikabidhi zawadi ya picha inayoonyesha nyumbu wanaovuka Mto Mara katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa Makamu wa Rais wa Cuba, Salvador Valdes Mesa, baada ya mazungumzo yaliyofanyika, Havana nchini Cuba, juzi. Kushoto ni Balozi wa Tanzania nchini humo, Humphrey Polepole. **PICHA: OWM**

# Mil. 700/- kuunganisha umeme kaya 2,800

**Na Benny Kingson,** TABORA

ZAIDI ya Sh. milioni 698 zimetengwa na Shirika la Umeme (TANESCO) kusambaza umeme katika vitongoji 45 vya Manispaa ya Tabora vyenye kaya 2,854.

Mratibu wa mradi wa REA wa shirika hilo Manispaa ya Tabora, Benedict Peter, alibainisha hayo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani. Kati ya vitongoji hivyo, 15 vimechaguliwa na Mbunge wa Tabora Mjini na 30 vimeteuliwa na serikali.

Peter alitaja vitongoji 15 vilivyochaguliwa na Mbunge Emmanuel Mwakasaka kuwa ni Chane, Igombe Mashariki, Kaloleni, Kagera, Mapambano, Kadoke, Kipera, Mtakuja Magharibi, Igombanilo, Kipalapala Mashariki, Mtakuja Mashariki, Ilobi, Kipalapala Magharibi, Usenge na Tiara.

Alitaja vitongoji vilivyoteuliwa na serikali ni pamoja na Ngemo, Malumba, Umanda Mashariki, Kipalapala Kaskazini, Tumbi. Kalatuma, Utembwa, Kilumbo, Mshikamano, Ibangu, Masimba, Nyakato, Isalalo, Lukombe, Iyombo Na.8, Shimo la Udongo, Kapande, Kapunze B na Amkeni.

"Vitongiji vingine ni Maendeleo, Imalauduki, Utyatya, Sokoine, Ugawe A, Kigombe, Ufunga, Tiara, Kapunze C, Kipela Kaskazini na Kakurungu ambapo vyote tutaviunganishia umeme kama tulivyopokea maelekezo toka serikalini na kazi hii itafanyika kwa umakini mkubwa," alisema.

> **"Vitongiji vingine ni Maendeleo, Imalauduki, Utyatya, Sokoine, Ugawe A, Kigombe, Ufunga, Tiara, Kapunze C, Kipela Kaskazini na Kakurungu ambapo..."**

Katika kikao hicho, ilielezwa pia kuwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Manispaa ya Tabora umeidhinisha jumla ya Sh. bilioni 2.23 kwa mwaka wa fedha 2024/25; wakala huo tayari una rukhsa ya kufanya ununuzi kwa asilimia 60 ya fedha hizo.

Meneja wakala huo, Subira Manyama, akiwasilisha taarifa yake katika Baraza la Madiwani, alisema kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/24 walitekeleza mikataba tisa kwa asilimia 84.78; walipata changamoto ya ucheleweshwaji wa matengenezo ya barabara kutokana na mvua.

"Changamoto nyingine ni makandarasi wamekuwa na mitambo michache isiyokidhi mahitaji kwa kuwa wamekuwa na kazi katika maeneo mengine, kuwa na mitaji midogo na uzembe kazini nako kulikuwa tatizo, tumeendelea kuwabana kwa kuzingatia mikataba yao," alisema.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) iliwasilisha mada kuhusu madhara ya rushwa katika uchaguzi, ikieleza kuwa kuharibu uchaguzi, kukosekana haki ya kupiga kura na kuchagua viongozi waadilifu kunachelewesha maendeleo ya jamii na serikali kwa ujumla.

Ofisa wa taasisi hiyo, Happnes Madege, alisema rushwa inadhalilisha utu wa wananchi, kuwaongopea na kuwapotezea dira na mipango mikakati ya maendeleo endelevu.

Baraza hilo limeazimia kuongeza zaidi mapato kwa kutafuta wawekezaji katika maeneo ya stendi ya zamani, eneo la PPP na sanamu la Mwalimu Nyerere pamoja na maeneo mengine muhimu wakati Tabora ikiwa katka mikakati ya kuwa jiji.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Wataka kiangaliwe chanzo utovu wa maadili

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BAADHI ya wakazi wa Mkoa wa Pwani, wameomba kiangaliwe chanzo kinachosababisha Watanzania kubadilika na kuingia kwenye mambo yanayochangia ongezeko la utovu wa maadili.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Pwani, Mwinshehe Mlao, alisema hayo alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha kamati ya ushauri ya mkoa huo kilicholenga kutoa maoni ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Mlao katika maoni yake alisema Dira ya Taifa inatakiwa kuangalia zaidi chanzo kinachosababisha watu wabadilike na kuacha mambo ya asili ya Tanzania.

Kadhalika, alisema kuimarishwa kwa umoja na mshikamano kwa wananchi inasaidia kuondoa mifarakano kati ya wananchi wenyewe kwa wenyewe.

Pia, amependekeza suala la kilimo cha umwagiliaji kwa mkoa huo ili wananchi wapate chakula muda wote tofauti na ilivyo sasa kuna ushirika mmoja ambao unajishughulisha na kilimo cha umwagiliaji.

Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Hamis Mtupa, amesema katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ni vema likazingatiwa suala la kuunganisha wilaya za mkoa huo kwa barabara.

Pia, Mtupa alipendekeza uboreshaji wa Bandari ya Mafia na kuwa na uwanja wa ndege wa uhakika katika wilaya hiyo tofauti na ilivyo sasa.

Washiriki wengine wa kikao hicho walitoa maoni ya Watanzania kuandaliwa kwa maisha ya baadaye wakiwa bado shuleni ili waweze kujiajiri badala ya kutengemea kuajiriwa.

Karimu Pazi, mmoja wa vijana wakulima kutoka Wilaya ya Kibaha, alitoa maoni kwa serikali kuwekeza nguvu kwenye kilimo chenye tija ili vijana waweze kujiajiri na kuwapatia mitaji.

Kadhalika, Ngobere Msamau ambaye ni mwenyekiti wa wafugaji amependekeza kuwa na ufugaji wenye tija kwa kuwa na miundombinu rafiki ikiwamo majosho na sehemu za malisho.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliwasisitiza wananchi wa mkoa huo kutoa maoni yao kwa kuwa sera hiyo haijinasibishi na itikadi ya chama badala yake ni maendeleo ya kila Mtanzania.

Kunenge alisema malengo yake ni kuona wakazi wa mkoa huo wakitoa maoni yenye tija kwa ajili ya vizazi vijavyo, ambayo yatatumika katika Dira ya Taifa ya Maendeleo.




Wananchi waliojitokeza katika kambi ya siku tatu ya upimaji wa afya bure katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana, wakipatiwa huduma na madaktari bingwa kutoka hospitali zinazomilikiwa na Jumuiya ya Khoja Shia Ithnasheer, ambao ni waandaaji wa kambi hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Malamba Mawili waomba eneo la kuzikia

**Na Pilly Kigome**

BAADHI ya wakazi wa Mtaa wa Zebra, Malamba Mawili, Kata ya Msigani Jimbo la Kibamba wameiangukia serikali wapatiwe eneo la kuzikia wapendwa wao kutokana na ukosefu wa eneo la huduma hiyo.

Hali hiyo inasababisha wengine kusafirisha wapendwa wao huku wengine wakihamisha maziko umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.

Maombi hayo waliyatoa jana mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alipokuwa akisikiliza kero za wakazi wa jimbo hilo katika viwanja vya Makuti Msigani jijini Dar es Salaam.

Wakizungumza na Nipashe baada ya kuwasilisha kero hiyo wakazi hao wawili waliokataa kutaja majina yao na mwingine Julius Msemo, walisema wana uhitaji mkubwa wa eneo hilo kwa kuwa, sasa imekuwa ni kadhia kubwa kwa kukosa eneo la huduma hiyo muhimu kwa kipindi kinachoelekea mwaka wa tano sasa.

Msemo alisema wanalazimika kuhamisha maziko kwenda umbali mrefu kutafuta huduma hiyo wangeweza kuwa na eneo wangeondokana na kadhia hiyo.

Aidha, wengine wanalazimika kusitiri ndugu zao chini ya nguzo za umeme kwa wanaokosa uwezo wa kusafirisha misiba kwenda umbali mrefu. "Leo tumefurahi sana rais wa Dar es Salaam ametufikia huku na tumemfikishia kilio chetu naamini atatusaidia kwani yeye ndiye mwenye dhamana ya kusaidia wakazi wake," alisema mmoja wa wananchi hao.

**"Leo tumefurahi sana rais wa Dar es Salaam ametufikia huku na tumemfikishia kilio chetu naamini atatusaidia kwani yeye ndiye mwenye dhamana ya kusaidia wakazi wake," alise-**

RC Chalamila amemwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo kutafuta na kutenga eneo hilo kwa haraka kwa wakazi hao.

Wakati huohuo, Chalamila alitangaza kuwachukulia hatua kali wazazi wote wanaoleta mzaha kwenye malezi ya watoto wao shuleni kwa kuwakosesha huduma muhimu wanafunzi wawapo shuleni.

Chalamila alionekana kuchukizwa na kuwatangazia wazazi wanaogoma kuwapa watoto wao fedha za uchangiaji wa chakula wawapo shuleni kwa kuwa hali hiyo inasababisha wanafunzi kudanganyika na kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja kutokana na kukosa fedha za chakula waendapo shuleni.

"Wazazi acheni mzaha juu ya malezi ya watoto wenu ni wajibu wenu kuchangia fedha za chakula kwa ajili ya watoto wenu ili mtoto aweze kuelewa vizuri masomo yake awapo darasani, msidanganyike na siasa za ovyo na maneno ya uzushi mitaani kuwa msichangie kwani elimu ni bure acheni mizaha," alisema.

Aliwataka wazazi kufundisha na kusimamia uvaaji mzuri kwa watoto ili kuwaepusha na kujihusisha na mapenzi katika umri mdogo na kuwa chanzo cha kusababisha ziro nyingi katika matokeo yao.

Chalamila alitoa agizo hilo baada ya kutoridhishwa na ufaulu wa wanafunzi kwa matokeo ya kidato cha nne ya mwaka 2023 na kati ya wanafunzi 353, waliopata ziro walikuwa ni 99.

Awali, alikagua miradi mbalimbali ukiwamo mradi wa nyumba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ubungo iliyogharimu Sh. milion 593.9 na barabara ya Matosa-Temboni yenye urefu wa kilomita tatu pamoja na kukagua mradi wa maji katika Kata ya Kwembe.

# Madereva Watanzania waeleza adha kufungwa mpaka Zambia, DRC

**Na Maulid Mmbaga**

MADEREVA wa Tanzania wanaosafirisha mizigo kwenda mataifa mbalimbali Afrika kwa kutumia magari makubwa (malori) wameeleza adha walizokutana nazo baada ya kufungwa kwa mpaka wa Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ikiwamo kuibiwa mafuta na vifaa vya gari.

Zambia ilifunga vituo vitatu vya mpaka wa Kasumbalesa kwa siku tatu kwa madai ya kutozingatiwa kwa mikataba ya kibiashara kati ya pande hizo mbili, ikiwamo kupinga uamuzi uliochukuliwa Julai, mwaka huu wa kupiga marufuku uingizaji wa bia na vinywaji baridi kutoka nje ya DRC.

Akizungumza na gazeti hili, mmoja wa madereva hao John Lyaheja, alisema mpaka huo ni wa pili kwa ukubwa baada ya wa Kinshasa na ukifungwa hata kwa siku moja madhara yanakuwa makubwa kwa wasafirishaji wa mizigo wanaovuka kutoka nchi moja kwenda nyingine.

Alisema magari ya mizigo kutoka nchi zaidi ya sita yanatumia mpaka huo na kwamba kutokana na kufungwa kwa siku tatu ilisababisha kutokea msongamano mkubwa na kuwasababishia walazimike kulala barabarani ikiwa ni maeneo ambayo hawawezi kijihakikishaia usalama wao.

"Hii pia inasababisha sisi madereva kuibiwa sana mafuta na vifaa vingine kutokana na kusimama sehemu moja kwa muda mrefu, inatulazimu kugeuka walinzi, foleni ya magari kwa upande wa Zambia ilikuwa ndefu karibu kilomita 50, huduma za vyoo pia hakuna hali inayotulazimu kwenda porini, hiyo ilisababisha dereva mmoja kufariki baada ya kung'atwa na nyoka," alisema Lyaheja.

Pia alitoa wito kwa mataifa hayo mawili kuweka miongozo mizuri na kuhakikisha changamoto hiyo haijitokezi tena kwakuwa kufungwa kwa mpaka inasababisha madhara makubwa ikiwamo kupoteza muda mwingi barabarani wakiwa kwenye foleni.

Aidha, ililezwa kuwa, licha ya kufanyika jitihada za kufunguliwa kwa mpaka huo baada ya mkutano kati ya waziri wa Biashara wa Kongo na mwenzake wa Zambia, hali bado haijarudi kuwa ya kawaida kutokana na msongamano mkubwa wa magari uliojitokeza kwa siku tatu wakati mpaka huo ukiwa umefungwa.

Waziri wa Biashara wa Kongo, Julien Paluku, alisema kuwa DRC haijakiuka makubaliano hayo. Marufuku ya bia na vinywaji baridi inahusu bidhaa kutoka nchi zingine, tofauti na Zambia.

"Bidhaa tu ambazo ni kutoka Zambia ndizo zinazonufaika na fursa. Na ninawaambie kuwa usafirishaji katika nchi zote zinazotuzunguka husababisha DRC kupoteza karibu dola bilioni tano (Sh. trilioni 13.5) kila mwaka," alisema.

Waziri wa Biashara na Viwanda wa Zambia, Chipoka Mulenga, katika taarifa yake alisisitiza kuheshimiwa kwa mikataba ya kibiashara inayohusu pande zote mbili.



# Wizara yakusanya taarifa milioni 12 anwani za makazi nchini

**Na Allan Isack**, ARUSHA

WIZARA ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imekusanya taarifa za anwani za makazi zaidi ya milioni 12 nchini.

Takwimu hizo zilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu Wizara hiyo, Nicholaus Mkapa, wakati akizungumzia operesheni ya kukusanya taarifa hizo milioni 12.3 iliyofanyika nchini.

Mkapa aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya ufunguzi wa uhakiki wa taarifa za anwani hizo kwa Mkoa wa Arusha.

Alisema utekelezaji wa mfumo wa anwani hizo unafanyika nchini kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003, makubaliano ya kikanda na kimataifa ya Umoja wa Posta Afrika na Duniani ambayo Tanzania ni nchi mwanachama.

Hata hivyo, alisema wizara hiyo imeandaa mkakati wa kufanya uhakiki wa taarifa katika halmashauri zote nchini na kuwajenga uwezo wataalamu, wenyeviti na maofisa watendaji kata na mitaa.

Alisema hadi sasa wamefanya uhakiki na kuwajengea uwezo wahusika katika halmashauri 31 nchini, kati ya hizo 19 ni za Bara na 11 Zanziba.

**Alisema wamefanikisha kuhuisha zaidi ya taarifa za anwani milioni 2.3, kutoa anwani mpya zaidi ya 500,000 na kuwajenga..**

Alisema wamefanikisha kuhuisha zaidi ya taarifa za anwani milioni 2.3, kutoa anwani mpya zaidi ya 500,000 na kuwajenga uwezo wataalamu, wenyeviti na maofisa hao watendaji wanaokadiriwa kufikia 6,621.

Kwa mujibu wa Naibu Katibu Mkuu huyo, wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 imejipanga kununua vishikwambi 3,422 kwa watendaji wa mitaa kwa ajili ya kusajili anwani mpya, kuhuisha taarifa na kutoa barua za utambulisho wa wakazi.

Mkurugenzi wa Huduma za Mawasiliano wa Wizara hiyo, Mulembwa Munaku, alisema lengo la operesheni hiyo ni kumwezesha kila mwananchi kutambulika mahali anapotaka kufikishiwa huduma kwenye makazi, ofisi au eneo la biashara.

Munaku, alisema kupitia operesheni hiyo, Arusha umekusanya taarifa na kutoa anwani za makazi 442,912 kwa wananchi.

Awali Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa huo, David Lyamongi, alisema mafunzo hayo yanahudhuriwa na wenyeviti wa mitaa wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, watendaji wa kata, mitaa, maofisa tarafa na wakuu wa idara.



Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambaye ni mlezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Manyara, Zubeir Ali Maulid (kushoto), akisalimiana na Mbunge wa Kiteto, Edward Ole Lekaita, alipofanya ziara ya kukagua uhai wa chama hicho na kuzungumza na wanachama katika eneo la Kibaya, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Madaktari bingwa wapiga kambi Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKAZI wilayani hapa Mkoa wa Tanga, wanatarajia kuanza kupatiwa huduma za matibabu bure na timu ya madaktari bingwa kutoka Taasisi ya Modewji Foundation ili kuhakikisha wanakuwa na afya bora.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Muheza Tanga, Zainab Abdallah, katika kikao kazi cha maandalizi ya kambi ya macho itakayoendeshwa na taasisi hiyo kwa siku tatu kuanzia kesho.

Zainabu alisema kuwa madaktari hao wataanza kutoa huduma hiyo kwa wananchi kuanzia Agosti 16 hadi 18, mwaka huu katika Hospitali ya Samia District Medical iliyopo Kata ya Lusanga.

" Nichukue fursa hii niwashukuru sana wenzetu wa Taasisi ya Modewji Foundation kwa kuamua kurudi kwa jamii na kutoa huduma muhimu zinazogusa maisha ya watu, Mungu awabariki sana," alisema.

Zainabu, alisema timu ya madaktari hao imejipanga kuwahudumia wananchi watakaojitokeza kwenye kambi hiyo kwa wakati.

Alisema watakaohitaji upasuaji huduma hiyo itakuwapo, kisha kufuatiwa na ufatiliaji wa maendeleo ya afya.

Mratibu wa maandalizi wa kambi hiyo wilayani hapa, Makame Seif, alisema maandalizi yote yamekamilika na kinachofanyika ni kuendelea kuhamasisha wananchi kupitia matangazo kwa kutumia vipaza sauti, wajitokeze kwa wingi kupata huduma hiyo bure.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Jumaa Mhina, alitumia kikao cha baraza la madiwani kuwakaribisha wawakilishi hao wa wananchi kujitokeza kwenye kambi hiyo kupima afya bure.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Mohamed Mfaki, alitoa rai kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kwenye kambi hiyo ili wajue afya zao na kupatiwa matibabu bure.

Diwani wa Kata ya Lusanga, Antony Kabulwa, alisema amekwisha kuhamasisha wapigakura wake kufika katika kambi hiyo kupata matibabu bure.

# Wanafunzi waiangukia serikali taulo za kike

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Arusha wameomba serikali kuweka taulo za kike kwenye orodha ya bidhaa muhimu ili kuwapunguzia gharama wanapopata hedhi.

Ombi hilo lilitolewa jana jijini hapa na mwanafunzi, Doreen Kowelo wakati wa kampeni ya uchangiaji wa taulo za kike iliyofanywa na msichana Arjun Mittal iliyojulikana kwa jina la "Her Needs Tanzania'.

Lengo lilikuwa ni kupata kiasi cha Dola za Marekani zaidi ya 60,000 kutoka kwa marafiki zake wa ndani na nje ya nchi ili kusaidia wasichana wapate hedhi salama.

Doreen, lisema endapo bidhaa hizo zitawekwa kwenye orodha muhimu, bei yake itashuka na kuwawezesha wasichana wengi kuzitumia.

" Baadhi yetu hatutumii taulo hizi kwa kuwa zinauzwa Shilingi 2,000 na wakati mwingine bei hiyo inakuwa juu zaidi kulingana na kampuni. Serikali ikitoa kauli ya bei kuwa moja na ya chini, wasichana wote tutaweza kutumia taulo hizi," alisema.

Mkurugenzi wa Kampuni ya HansPaul, Satbir HansPaul, alimpongeza Arjun Mittal, kwa kuonyesha mfano wa kuchangia wasichana hao, wakiwamo wanaoishi maeneo ya pembezoni wapate fursa ya kuhudhuria vipindi shuleni, wakiwa na uhakika wa kupata taulo hizo.

"Tuwaunge mkono watoto hawa kupitia kampeni hii, wanafunzi wengi wa kike wapate taulo hizi na kufurahia masomo wakiwa na uhakika zaidi na furaha," alisema.

Kwa upande wake, Arjun, aliomba wadau kuchangia kampeni hiyo ili aweze kuwafikia wasichana zaidi ya 40,000 na kwa awamu ya kwanza.

# TAKUKURU yawapiga msasa waandishi Kilimanjaro

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAANDISHI wa habari mkoani Kilimanjaro wameshauriwa kuibua vitendo na viashiria vya rushwa kuelekea katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani.

Ushauri huo ulitolewa jana na Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kilimanjaro, Mussa Chaulo, kwa waandishi hao katika mafunzo yaliyoandaliwa na taasisi hiyo ya kuwajengea uwezo wa kubaini vitendo hivyo katika chaguzi hizo zitakazovishirikisha vyama vingi vya siasa nchini.

Chaulo alifafanua kuwa ametoa rai hiyo baada ya taasisi hiyo kubaini kuwa wanahabari wanatumika kuleta ubaguzi, uchochezi, chuki na kukwamisha maendeleo.

"Vyombo vya habari ni nguzo muhimu kufichua rushwa katika jamii ili kuhakikisha kila mwananchi anapata haki stahiki, hakikisheni hamtumiki vibaya," alisema.

Alisema katika kipindi hiki cha kuelekea chaguzi hizo watajitokeza wanasiasa wengi na kujifanya wapo karibu nao kwa lengo la kuwanunua kwa manufaa binafsi.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Kilimanjaro, Bahati Nyakiraria, aliitaka taasisi hiyo kutoa mafunzo hayo mara kwa mara kwa kada tofauti ya waandishi kwa lengo la kuwajengea uwezo.





# TAKUKURU yatibua hujuma bilioni 3/- ujenzi wa soko, stendi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Tabora imebaini hujuma ya zaidi Sh. bilioni 3 katika mradi wa ujenzi wa stendi na Soko Kuu la Manispaa ya Tabora.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tabora, Abnery Mganga, juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu taarifa ya utekelezaji wa taasisi hiyo kwa kipindi cha miezi mitatu.

Mganga, alisema katika uchunguzi uliofanyika kwa kipindi hicho, taasisi hiyo imebaini kuna watu walitaka kuhujumu zabuni ili kujipatia kiasi hicho cha fedha zaidi ya Sh. bilioni 3.053.

Alisema mradi huo wa Stendi ya Inala na Soko Kuu la Manispaa ya Tabora, ulipangwa kutumia Sh. bilioni 16 hadi kukamilika kwake, lakini watu hao (hakuwataja) walitaka kujiongezea kiasi hicho ili wajipatie fedha hizo kwa njia haramu.

Mganga, alisema TAKUKURU baada ya kubaini mpango huo ilifanikiwa kuzuia jaribio hilo na kuokoa fedha hizo.

Alisema TAKUKURU inaendelea na uchunguzi ili kuwachukulia hatua za kisheria kwa watu hao, ikiwa ni pamoja na kuwakamata na kuwafikisha mahakamani kujibu mashtaka ya kuhujumu fedha katika zabuni hiyo.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi (mbele), akikagua jengo la bweni la Shule ya Sekondari Ngoreme, juzi. Alitoa wiki sita kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, Dk. Maulid Madeni, kukamilisha ujenzi wa bweni hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi wakumbushwa malezi ya wahitimu msingi, sekondari

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA) imewataka wazazi na walezi kusimamia malezi bora kwa watoto wao baada ya kuhitimu elimu ya msingi na sekondari ili kudhibiti mmomonyoko wa maadili wanapokuwa uraiani.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi ya Elimu TEA, Masozi Nyirenda, wakati wa mahafali ya 20 ya darasa la saba katika Shule ya Rocken Hill Academy na ya kidato cha nne ya Shule ya Sekondari ya Anderlek Ridges yaliyofanyika Kata ya Mwendakulima Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga. Nyirenda, alisema baada ya masomo yao ya msingi na sekondari, baadhi ya watoto wamekuwa wakijiingiza katika vitendo viovu kinyume na maadili ya Watanzania ikiwamo ulawiti, matumizi ya dawa za kulevya, mimba na ndoa za utotoni.

"Kila mzazi ana wajibu wa kumlea mtoto wake katika maadili mema ili kumkinga kujihusisha katika vitendo viovu. Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalumu kwa kushirikiana na vyombo vya dola imekuwa ikipiga kelele juu ya suala la malezi kila kukicha na mengi yamekuwa yakiibuka kwenye jamii na wanaofanya ni vijana," alisema Nyirenda.

Alisema walimu wanatekeleza wajibu wao ipasavyo kumlea mtoto awapo shuleni, wanamkabidhi akiwa na nidhamu, lakini cha kusikitisha anaharibikia mikononi mwa mzazi baada ya kukutana na makundi ya mitaani. Mkurugenzi Mkuu wa shule hizo, Alexander Kazimil, alisema wamewafundisha maadili mema vijana wote namna ya kuishi na watu kwenye jamii zinazowazunguka na kutojihusisha na makundi yenye viashiria vya matendo maovu. Kazimil, alimtaka kila mzazi kuwa na wajibu wa kumlea mwanawe badala ya kuwaachia walimu pekee.

Mmoja wa wazazi wa wahitimu hao, Matha Samwel, alisema watoto wao wengi wanaathirika kisaikolojia baada ya kuhitimu elimu ya msingi, sekondari na kupata uhuru wa kupitiliza.

# Walimu watakiwa kuzingatia nidhamu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga mkoani hapa, Alexius Kagunze, amewataka walimu wa sekondari kuzingatia nidhamu na maadili ili kuboresha kiwango cha elimu wilayani humo.

Kagunze alitoa wito huo juzi kwenye kikao kazi cha walimu wa sekondari kilichofanyika Shule ya Msingi Buhangija cha kupanga mikakati ya kuhakikiha wanafunzi wanapata elimu bora na kuzalisha taifa la wasomi.

Alikemea tabia ya baadhi ya wakuu wa shule za sekondari kutumia madaraka yao vibaya kuwakandamiza walimu wengine na kuwa chanzo cha kukwamisha utendaji wao wa kazi.

Ofisa Elimu wa Sekondari wa Halmashauri hiyo, Lucas Mzungu, aliahidi kuwasimamia walimu na kuwakumbusha miiko ya kazi ili kufikia malengo waliyojiwekea ya kuinua kiwango cha elimu.

# Serikali kuendelea kushirikiana na wawekezaji nchini

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MKUU wa Wilaya ya Tarime mkoani Mara, Maulid Surumbu amesema serikali itaendelea kushirikiana na wawekezaji katika sekta ya madini wilayani hapa ili kuimarisha uhusiano na wananchi wanaozunguka maeneo yao.

Surumbu alisema mahusiano kati ya mwekezaji mwenye hisa na serikali, Barrick North Mara na wakazi wanaoishi vijiji jirani, yamesaidia kupatikana huduma za jamii kama vile elimu, afya na maji kwa wananchi.

Akizungumza katika tamasha la michezo lililoandaliwa na mgodi huo kwa ajili ya kuwawezesha vijana kuonesha vipaji vyao kutoka vijiji vinavyozunguka eneo la uwekezaji alisema kuwa: "Tukihakikisha uwepo wa Barrick ni nguvu chanya inayokuza jumuiya imara kiuchumi kwa wananchi."

Meneja wa Barrick North Mara, Apolinary Lyambiko, alisema kampuni hiyo inaendesha uchimbaji madini kwa uadilifu na kutoa taarifa juu ya shughuli zake nchini.

"Lengo letu ni kushirikiana na jamii inayozunguka kwa kuimarisha mawasilisho ya kila siku ili kusaidia kustawi," alisema Lyambiko.

ama
ALHAMISI AGOSTI 15, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Machimbo jina la mtaa linaloakisi uchafuzi mazingira, makazi duni**



**Viumbe hawa wanaweza kugundua maradhi yanayosumbua wanadamu**

Ukurasa 14

## WAFAMASIA:

# Acheni matumizi holela ya dawa mnayaweka maisha yenu rehani

• Chanzo magonjwa ya figo, ini usugu wa vimelea, kutokutibika

**Na Beatrice Moses**

NI mazoea kununua dawa kiholela kuanzia 'flajili' unaposikia tumbo linauma au kuhara na 'antibayotiki' kubwa kama 'amoksilini na azuma' hata bila kumwona daktari.

Mtindo uliozoeleka, ni kwenda kwenye duka la dawa, kununua au kueleza shida yako. Na bila kujali, mwingine humeza vidonge vichache na baadhi hutumia nusu dozi na kuachana na dawa baada ya kupona.

Wataalamu wa afya wanathibitisha kwamba, mazoea ya kumeza dawa pasipo maelekezo wala vipimo sahihi, ni kujimaliza, wapo watu kadhaa imewagharimu maisha baada ya kuwasababishia maradhi ya ini na figo.

Hapa wataalamu hao wanaonya kuwa, kununua dawa na kujitibu kiholela ni hatari, kwa kuwa dawa za tiba sio sawa na bidhaa nyingine, umewekwa utaratibu maalum wa kufuatwa, ili kusimamia matumizi sahihi na kudhibiti hatari na athari za kiafya zinazoweza kujitokeza.

Baraza la Famasi lililopo chini ya Wizara ya Afya, kupitia kipeperushi chake linaelimisha matumizi sahihi ya dawa kuwa ni sumu na huleta madhara iwapo hazitatumiwa ipasavyo.

Linasema ni muhimu mgonjwa kufanyiwa uchunguzi na kupata ushauri wa mtaalam wa afya kabla ya kutumia dawa.

**MAANA YA DAWA**

Ni kemikali au kitu chochote kinachotumika kutibu au kuzuia ama kutambua magonjwa ya binadamu au wanyama. Zinaweza kuwa vidonge, za maji na mafuta, gesi, hewa ya kuvuta na mionzi.

Baraza linasema zinaweza kutumiwa kwa njia mbalimbali kama kumeza vidonge, kunywa dawa za maji, kupaka, kuchoma sindano na kuvuta kwa njia ya hewa.

Matumizi sahihi ya dawa, kwa mujibu wa Baraza la Wafamasia, yanahusisha mgonjwa kufanyiwa uchunguzi wa kina, kuandikiwa na kupewa dawa anayostahili kulingana na hali ya ugonjwa wake.

Anaelekezwa kutumia dawa kwa kipimo, njia na muda sahihi kulingana na maelekezo aliyopewa na mtaalam wa afya.


Pia matumizi sahihi ya dawa yanazingatia uhifadhi wa dawa katika kipindi chote cha matibabu anayopokea.

Kwa mujibu wa baraza hilo, ni kujinunulia na kutumia dawa pasipo maelekezo ya mtalaam wa afya, kutokumaliza dozi au dozi kamili na kuchangia dawa na mtu mwingine.

**ATHARI ZAKE**

Madhara ya matumizi yasiyo sahihi ya dawa, ni pamoja na kuongezeka ugonjwa, kutopata nafuu, kutopona hatimaye kufa.

Mengine yanatajwa kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na kusababisha maradhi ya figo na ini kuwa na jamii isiyo na imani na mfumo wa kutoa huduma za afya.



Mteja akihudumiwa kwenye duka la dawa. **PICHA: BEATRICE MOSES**

Baraza la Famasi linatahadharisha watu kuepuka kununua dawa kwenye maduka yasiyosajiliwa kisheria, kwa kuwa ubora wake ni wa mashaka, pia maelezo ya matumizi yanaweza kutolewa bila usahihi au na mtu asiye sahihi, kitendo kinachoweza kusababisha madhara kwa mtumiaji.

Matumizi sahihi ya dawa, yanapunguza usugu wa vimelea vya ugonjwa na kiasi cha madhara na maudhi ya dawa inayotumika. Kwa upande mwingine huipunguzia serikali au gonjwa gharama za matibabu.

Hupunguza uwezekano wa kupata magonjwa yanayoweza kusababishwa na matumizi holela ya dawa, huboresha afya ya mgonjwa kwa kupona kwa wakati na kujenga imani kwenye mfumo wa kutoa huduma wa afya na wataalamu wake, linasema Baraza la Famasi.

Ikumbukwe, awali huduma za dawa katika maduka ya dawa muhimu ilitolewa kwa mujibu wa Sheria ya Dawa na Sumu ya mwaka 1978, ambayo baada ya utafiti ilifutwa.

Wakati huu huduma inatolewa kwa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003. Maduka ya dawa muhimu yaliyoanzishwa na kusajiliwa na mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), ndio yaliyoruhusiwa kutunza na kuuza dawa, kabla ya mabadiliko kufanywa.

Baada ya kutungwa kwa Sheria ya Famasi ya mwaka 2011, TFDA inabaki na mamlaka ya kusimamia na kudhiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa.

Mkuu wa Kitengo cha Sheria Baraza la Famasi Paulo Makanja, anasema, kwa mujibu wa Sheria ya Famasi, baraza hilo ndilo lenye wajibu wa usimamizi na udhibiti wa maduka ya dawa muhimu.

Anabainisha kuwa vifungu vya 45 na 48 vinatoa wigo wa utendaji kazi, kulingana na vigezo na inaeleza adhabu zinazotolewa iwapo mtoa huduma za dawa atakwenda kinyume.

"Kwenye duka la dawa inapaswa kuwekwa cheti cha muuzaji ili iwe rahisi kutambua kiwango chake cha elimu na dawa anazouza. Hii ni muhimu ndio maana wakaguzi hukagua ili kujiridhisha," anasema Makanja.

Anasema, muuza dawa au mgawaji anapaswa kuwa na mafunzo ambayo yanatambulika, hivyo kwenye kila duka la dawa muhimu na famasi kunapaswa kubandikwa vyeti vya muuzaji ili kuonyesha

Inaendelea Uk. 12

AFYA

# Machimbo jina la mtaa linaloakisi uchafuzi mazingira, makazi duni

Na Mwandishi Wetu

USAFI wa mazingira na ulinzi shirikishi ni mambo yanayowahitaji wananchi kuchangia fedha za kulipa makandarasi wanaosafisha na sungusungu wanaowalinda usiku, ni jambo lisilokubalika kwa baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam.

Eneo mojawapo ni Mtaa wa Machimbo uliopo Segerea wilayani Ilala, huko kinachotokea ni baadhi ya wakazi kukaidi kulipa ada ya kuzoa taka na ya ulinzi shirikishi pia.

Ukaidi huo husababisha maeneo ya wakorofi hao kukithiri uchafu na uhalifu hasa wizi na vibaka wanaoranda randa wakati wote.

Kukwepa kulipa ada hizo, kumesababisha mitaa wanakoishi wanaokataa kuchangia gharama kuitwa mtaa wa 'wagumu'.

Ni jina linalotumiwa na vijana waliopewa kazi ya kuzoa taka katika mtaa huo wa Machimbo wakati wakipeana ishara wanapofika kuhimiza kulipa ada hiyo.

Wafanyakazi hao wanadai kuwa kitendo hicho cha wagumu kinakwamisha kampeni ya kuweka mazingira ya mitaa kwenye usafi, kutokana na taka kuzagaa kwenye makazi yao na nyingine kutupwa majumba ambayo ujenzi wake haujakamilika hasa mapagale.



Maisha ya 'wagumu' wanaoishi Mtaa wa Machimbo Segerea. **PICHA: MWANDISHI WETU**

Ukifika Machimbo unakutana na taka zikiwa zimejaa kwenye viroba, nyingine hutelekezwa barabarani, vichochoroni, mitaroni, nje ya nyumba za watu na maeneo ya wazi, kama viwanja vya mpira na vya mafurushi hayo yakitupwa nyakati za usiku.

Ofisi ya mtaa huo na wafanyakazi wa kandarasi hizo, wanapita mitaani kuutangazia umma kwa vipaza sauti kuhamasisha wananchi kuzoa taka walizokusanya kwenye makazi yao.

Kitendo hicho kimezua malalamiko pia baadhi ya wakazi wa mitaa hiyo wanadai kudhalilishwa kwa kuitwa wa wagumu, wakisema wanatoa ushirikiano kwa kuchangia pesa baada ya kutangaziwa, lakini magari hayafiki kwenye makazi wanapozikusanya kutokana na ubovu wa barabara.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Machimbo, Mariamu Machicha, katika mikutano na wananchi hivi karibuni, anasema changamoto hiyo ni moja ya nyingi zinazoukabili mtaa wao.

Kwa mujibu wa Mariam amekuwa akiwahimiza wananchi kutoa ushirikiano kwa makandarasi na walinzi shirikishi kwa kukusanya taka na kuchangia walinzi.

Anasema pamoja na jitihada ambazo ofisi yake imekuwa ikifanya baada ya kupokea malalamiko, kukutana nao kwa kuwafuata kwenye makazi nao na mikutano ya hadhara, bado wapo ambao wanakaidi kulipa ada ya taka na kupelekea baadhi yao kukamatwa na kutozwa faini kwa kutupa taka ovyo.

"Mkandarasi chini ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ameondoa kero ya takataka kwa kiasi," anasema Mariam na kuongeza kuwa bado kuna malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi.

### MACHIMBONI NINI?

Baadhi ya wakazi wa Machimbo wanasema asili ya jina la Machimbo linatokana na mtaa huo katika miaka ya nyuma kutumika kuchimba mchanga ambao ulikuwa ukitumika kwenye ujenzi na kupiga matofali maeneo mengine Dar es Salaam.

Baadhi ya maeneo yaligeuka mashimo ambako kuna nyumba zimejengwa na kukabiliwa na chemichemi zinazotiririsha maji kwa mwaka mzima na kuwa kero kwa watu wanaoishi kwenye maeneo hayo.

Sehemu hizo zimekuwa vilindi vya maji taka kutoka vyooni na kuwa hatarini kukumbwa na magonjwa ya milipuko.

Akizungumzia kuhusu maji taka hayo, Mariam, anasema kamati ya mazingira ya mtaa, ofisa mtendaji kata na ofisa afya wanashirikiana kuondoa tatizo la maji yanayotiririshwa barabarani na kuzidi kukera wakati wa mvua.

Mariam anasema wanakagua kubaini ukweli wa malalamiko wanayopokea, kutoa maelekezo na wakati mwingine kuchukua hatua, lakini malalamiko bado yapo sehemu nyingine na yanayosababishwa na chemchemu.

### BARABARA

Akizungumzia barabara anasema Mtaa wa Machimbo una barabara moja iliyojigawa kwenye kuhudumia makazi na ofisi mbalimbali, lakini ingawa serikali iliiwekea kifusi bado kuna mashimo.

Aidha, anasema kamati ya mtaa imeendelea kupunguza mashimo kwa kuweka vifusi na kuvisambaza kwa nyakati hasa pale barabara zinaposhindikana kupitika.

Kuhusu utiririshaji maji taka barabarani, Mariam anasema nayo ni changamoto inayoukabili mtaa wa Machimbo na kuendelea kuchafua mazingira.

Anasema changamoto hiyo inasababishwa na maeneo mengi kukosa barabara za kuingia kwenye makazi kutokana na ujenzi holela, hivyo magari kushindwa kupita kwenye kutoa huduma ya kunyonya maji hayo na mengine baadhi ya mashimo kufurika.

"Kijiografia, maeneo mengi ya mtaa huu ni chemchem, pia kuna ujenzi holela wa makazi na kukosekana kwa barabara," anasema Mariam na kuongeza:

"Kutiririsha maji barabarani kumesababisha barabara nyingi kuharibika na kubaki mashimo, adha ya usafiri kwenda kwenye makazi ya watu kutokana na magari kushindwa kupita."

Anasema barabara nyingi za Machimbo zimeharibika vibaya na kupelekea wakati mwingine kutopitika kutokana na madereva kunusuru vyombo vyao na uharibifu.

### UHALIFU

Anaelezea kuwa kuna uhalifu na kutishia usalama akiitaja changamoto nyingine inayoukabili mtaa huo kuwa ni wananchi kukaidi kulipa ada ya ulinzi.

Mariam anasema ada hiyo ambayo ipo kwa mujibu wa sheria, ni fedha ambazo hutumika pamoja na mambo mengine kuwalipa askari jamii wanaolinda mtaa wake au makazi ya wananchi.

Anasema kitendo hicho kimechangia ulinzi 'kusinzia' kwenye baadhi ya maeneo, licha ya baadhi ya wananchi kulalamika kukithiri kwa vitendo vya wizi, ukiwamo wa kukata madirisha na kuiba simu, nguo na runinga.

Mtaa wa Machimbo kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, una watu 10,333 kati ya hao, wanawake 5,568 na wanaume 4,765.

# Acheni matumizi holela ya dawa mnayaweka maisha yenu rehani

**Inatoka Uk. 11**

uhalali wa uuzaji au utoaji wa dawa hizo katika utaratibu uliowekwa.

Mfamasia Irene Massawe kwenye duka la dawa Nakiete liliko Dar es Salaam, anasema wamekuwa wakipata changamoto kubwa kutoka kwa wateja wanaofika na kutaka kuuziwa dawa bila kuwa na cheti chenye maelekezo ya dawa wanazohitaji.

"Anafika dukani anakwambia nipe dawa ya malaria maana ninavyojisikia hii ni malaria tu, naujua mwili wangu hata unapomwambia kuwa anapaswa kupimwa ili kuwa na uhakika haelewi inawezekana akapewa dawa hizo, kisha kusisitizwa kuwa dalili zikiendelea aende hospitali," anasema.

Irene anaongeza kuwa kuna baadhi ya dawa za maumiivu, ambazo wanaruhusiwa kuuza bila cheti, lakini za magonjwa kama presha au kisukari, ambayo ni endelevu kwa mgonjwa huuzwa kwa tu kwa vyeti au maelekezo ya daktari.

Mratibu wa Kanda ya Mashariki wa Baraza la Famasi Arapha Nshau, anasema wafamasia watalam waliosajiliwa ni 3,789 na kwamba ni wale wenye elimu ya kiwango cha kuanzia shahada ya famasi.

Wengine ni fundi dawa sanifu wako 8,466 (stashahada ya famasia) pia kuna fundi dawa wasaidizi 1,042 wenye elimu ya awali ya famasi.

Nshau anasema, maduka makubwa ya dawa yanayoruhusiwa kuuza dawa na vifaa tiba mbalimbali yaliyosajiliwa ni 3,187, maduka ya dawa muhimu ni 22,536 ambayo kuna baadhi ya dawa hayaruhusiwi kuziuza. "Maduka haya ya dawa muhimu hupaswa kusajiliwa pembezoni mwa maeneo ambayo hakuna zahanati au kituo cha afya, lengo likiwa likiwa ni kurahisisha kupatikana kwa dawa muhimu za matibabu. Wanaruhusiwa kuuza aina 37 tu za dawa," anasema.

Vilevile, anakumbusha kuwa kuanzishwa kwa maduka haya ni kuimarisha kupatikana huduma bora za afya kwa wananchi, ikizingatiwa kuwa yanapaswa yasimamiwe na kuendeshwa na mtu aliyepata mafunzo ya msingi ya kutoa dawa.

Anasisitiza kuwa, yanapaswa kuanzishwa vijijini au miji midogo, ambako upatikanaji wa dawa ni tatizo, na kwamba ni sharti yaanzishwe katika umbali usiopungua mita 150 kutoka duka moja hadi jingine.

AFYA

# MSD inavyopambana Tanzania ijitegemee bidhaa za afya ikizizalisha nyumbani

**Na Restuta James**




Baadhi ya wafanyakazi wa kiwanda cha Idofi kinachozalisha glovu za uchunguzi, wakizihakiki kwa ajili ya kuzifungasha. **PICHA: RESTUTA JAMES**

KIWANGO kikubwa cha vifaa tiba pamoja na dawa zinazotumika nchini huagizwa kutoka nje, ni jambo linaloligusa Bohari ya Dawa (MSD), ikiazimia kufanya mabadiliko.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya, serikali inaagiza kutoka nje dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara kwa asilimia 86 na asilimia 14 pekee ya mahitaji hayo hupatikana nchini.

MSD yenye jukumu la kupunguza utegemezi huo wa bidhaa za afya, inasema baada ya marekebisho ya sheria inayounda bohari hiyo, imepewa uwezo wa kuzalisha, kununua, kuhifadhi na kusambaza bidhaa za afya na sasa itaanza kutekeleza jukumu hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, anapozungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, anasema ili kuondoa utegemezi huo, serikali imeipa mtaji wa Sh. bilioni 100.

Na sasa MSD inakusudia kushirikiana na wabia wenye fedha, teknolojia na uzoefu katika kuzalisha bidhaa za afya, ili lengo la taifa kujitosheleza litimie.

Tukai anasema ili kutekeleza sera ya viwanda, MSD imeanzisha kampuni tanzu ya Medipharm Manufacturing Company Limited, itakayosimamia shughuli za kuzalisha bidhaa zote za afya.

Kwa mujibu wa Tukai tayari bodi ya kampuni hiyo imeshazinduliwa sasa inasimamia viwanda vinavyozalisha bidhaa za afya, vinavyomilikiwa na MSD.

"Kampuni hii itaweza kuingia ubia na wawekezaji wengine. Kwa sasa, itasimamia kiwanda cha mipira ya mikono cha Idofi - Njombe, eneo la viwanda la Zegereni - Pwani na kiwanda cha barakoa - Dar es Salaam," anasema.

Anasema mipango inalenga viwanda vya Zegereni, vitazalisha dawa za aina mbalimbali, wakati kile cha Simiyu, kitazalisha bidhaa za pamba kama (gozi na mashuka), kwa ajili ya matumizi ya hospitali.

Kuwapata wawekezaji wenye uwezo wa kifedha, teknolojia na uzoefu, Tukai anasema MSD inafanya mawasiliano na balozi za Tanzania za China, Korea Kusini, Urusi na Algeria ili kuwatambua wazalishaji na wawekezaji wenye sifa hizo.

**VIWANDA VILIVYOPO**

Anasema viwanda vilivyopo ni kile cha barakoa kilichoko Keko, Dar es Salaam kinachozalisha barakoa za kawaida na maalum (N95). Anaongeza: "Kiwanda cha barakoa kimezalisha na kusambaza barakoa zenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni nne na kufanya nchi kujitosheleza kwa bidhaa hizo," anasema Tukai.

Anaongeza kuwa kiwanda cha kutengeneza mipira ya mikono au glovu, kimeanza kazi Februari mwaka huu na hadi Juni, kilikuwa kilitengeneza glovu milioni nne.

"Kiwanda hiki kimetoa ajira 136 kwa wakazi wa Makambako na kufanya ununuzi kwenye kampuni mbalimbali ziliozopo eneo hilo. Kwa kutengeneza mipira ya mikono ya kiuchunguzi pekee kiwanda kitaweza kuokoa zaidi ya Sh. bilioni 11," anasema.

Kaimu Meneja wa kiwanda hicho, Shiwa Mushi, anasema wanatarajia kuzalisha mipira ya uchunguzi au glovu hizo jozi milioni 86.4 kwa mwaka ambayo itakidhi mahitaji ya ndani kwa asilimia 83.4 kwa muda huo.

Anaeleza kuwa mahitaji ya mipira hiyo nchini ni jozi milioni 104 kwa mwaka hivyo, uzalishaji wa jozi milioni 86.4 utaokoa Sh. bilioni 20 kwa mwaka na kwamba malengo ni kuzalisha aina nyingine ya mipira hiyo kwa ajili ya wahudumu wanaofanya upasuaji, kazi yote ya uzalishaji inafanyika kwa umakini na kuzingatia ubora katika kila hatua kwa sababu bidhaa za afya zinahitaji usafi wa hali ya juu.

Tunazingatia vigezo vya ubora kama tulivyoelekezwa na mamlaka za udhibiti, anasema mbali ya viwanda vya Keko na Idofi, Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa MSD, Etty Kusiluka, anasema viwanda vya Zegereni na Simiyu, viko mbioni kuanza uzalishaji.

**UNUNUZI BIDHAA ZA AFYA**

Tukai anasema sambamba na ujenzi wa viwanda, bohari hiyo inajenga maghala ya kuhifadhi bidhaa za afya, ili kukidhi kasi ya uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali kwenye ujenzi wa vituo vya afya.

"Serikali kupitia Bohari ya Dawa imeanza ujenzi wa maghala ya kisasa katika Kanda ya Mtwara na Dodoma ili kukidhi upungufu uliojitokeza. Ujenzi huu ukikamilika utagharimu kiasi cha Sh. bilioni 40. Kwa sasa mradi umefikia asilimia 55 kwa ghala la Mtwara na asilimia 58 kwa ghala la Dodoma.

Kukamilika kwa ujenzi wa maghala kutasaidia kuimarisha uhifadhi wa bidhaa za afya kwenye viwango stahiki, kusogeza huduma karibu na vituo vya kutolea huduma za afya, kupunguza gharama za uhifadhi na kuimarisha utunzaji wake,"anasema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, ujenzi wa maghala hayo unatarajiwa kuongeza nafasi ya uhifadhi wa bidhaa za afya kwa mita za mraba 12,000 ambapo kwa ghala lililopo Dodoma mita za mraba 7,200 zitaongezeka na ghala la Mtwara mita za mraba 4,800 zitaongezeka hivyo kufanya ongezeko la uhifadhi kutoka mita za mraba 56,858.57 na kufikia mita za mraba 68,858.57.

Akizungumzia mapato, Tukai anasema maboresho yanayoendelea yamewezesha vituo vya kutolea huduma za afya kuwa na imani na utendaji wa MSD ambapo makusanyo ya fedha yameongezeka kutoka Sh. bilioni 40.3 mwaka 2022/23 na kufikia Sh. bilioni 118.9 kwa mwaka 2023/24.

Akieleza zaidi Tukai anasema kutokana na maboresho yanayoendelea kufanywa na Serikali, mapato ya Bohari ya Dawa yameendelea kuongezeka kutoka Sh. bilioni 359.6 kwa mwaka 2022/23, hadi zaidi ya Sh. bilioni 510.07 mwaka wa fedha 2023/24 likiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 150.43 ambayo ni sawa na asilimia 42.

Mkurugenzi Mkuu Tukai anasema mbali ya ujenzi wa viwanda, MSD imeongeza ununuzi wa bidhaa za afya kutoka kwa wazalishaji wa ndani ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/24, bidhaa za afya zenye thamani ya Sh. bilioni 22.1 zilinunuliwa kutoka kiasi cha Sh. bilioni 14.1 mwaka 2021/22 ikiwa ni ongezeko la asilimia 57.

"MSD imeendelea kufanya ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba vinavyohitajika katika vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya msingi hadi vituo vinavyotoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi nchini kama mashine za kusafisha damu , za uchunguzi MRI na CT- Scan, ultrasound, digital X-Ray pamoja na vitendanishi vyake.

Uwepo wa vifaa hivi unawezesha utambuzi wa magonjwa kwa usahihi na kutolewa kwa tiba sahihi," anasema, na kuongeza kuwa kununua kwa wingi katika viwanda vya ndani, kumeviongezea uzalishaji na kuvutia wawekezaji ambao watatengeneza ajira huku serikali ikiokoa fedha za kigeni, ambazo zingetumika kuagiza dawa nje ya nchi.

**MSD IRINGA**

Meneja wa MSD Kanda ya Iringa, Robert Lughembe, anasema ofisi yake inahudumia Halmashauri 17 zilizopo katika mikoa ya Iringa (5), Njombe (5) na Ruvuma (7).

Anasema huduma za MSD zimeboreshwa na sasa wanahudumia wateja mara sita (kila baada ya mwezi mmoja), badala ya mara nne kila baada ya miezi mitatu ya awali.

AFYA

# Viumbe hawa wanaweza kugundua maradhi yanayosumbua wanadamu

**Na Mwandishi Wetu**



LINAPOKUJA suala la kutambua ugonjwa kwa usahihi, unaweza kufikiri mara zote kuwa unahitaji mashine kama X-ray, CT Scan za gharama kubwa na vifaa vinavyoweza kuangalia kwa undani kile kinachotokea mwilini mwako.

Ingawa vifaa hivyo vinafanya kazi ya kushangaza, lakini sio pekee vinavyoweza kugundua maradhi yaliyoko tumboni, kichwani au kwenye mapafu.

Kuna matukio mengine ambayo wamiliki wa wanyama hugundua kwamba walikuwa na tatizo la kiafya kwa sababu ya viumbe hao.

Mifano hii, ni pamoja na mbwa kulamba, kunusa, na hata kujaribu kutafuna madoa kwenye ngozi ya wamiliki wao, ambayo baadaye hugunduliwa kuwa ni saratani ya ngozi.

Hawa ni baadhi ya wanyama ambao wanaweza kugundua maradhi kwa wanadamu, wanapofunzwa.

**MBWA**

Mbwa hutambua harufu fulani hata ikiwa iko katika kiwango cha chini sana. Huenda ni mfano unaojulikana zaidi wa mnyama anayeweza kutambua magonjwa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ule wa kutetemeka kutokana na matatizo ya ubongo, saratani ya kibofu cha mkojo na malaria.

Kifafa na kiwango cha chini cha sukari katika damu kwa wagonjwa wa kisukari vinaweza pia kufichuliwa na mbwa maalumu waliofunzwa.

Uwezo wa mbwa wa kutambua harufu ni muhimu katika kuzijua harufu fulani, hata ile ya kiwango kidogo au cha chini.

Inaaminika uwezo wa mbwa wa kunusa harufu, ni mara 10,000 zaidi ya ule wa binadamu. Wanaweza hata kutumia pua kuchunguza harufu mpya.

Mbwa wa tahadhari hufunzwa kutambua mabadiliko ya harufu au ya kimwili na kitabia kwa mlezi wao, ambayo yanatabiri kuwa na tatizo kama kifafa au shida nyingine ya kiafya.

Mbwa wa utambuzi kwa kawaida hushangaa wanapotambua kisha hutangamana na mhudumu wao, wakati mwingine huwapapasa au kuwagusa ili kuashiria wanahitaji kuchukua hatua kwa ajili ya usalama wao.

**PANYA**

Panya wana uwezo mahiri katika kugundua harufu fulani. Wapo panya wamepewa mafunzo ya kutambua harufu ya vilipuzi au mabomu ya ardhini nchini Msumbiji.

Pia wamethibitika kuwa na uwezo kwenye uchunguzi wa kimatibabu, hugundua maradhi ya kifua kikuu katika sampuli za makohozi ya watu wanaohisiwa kuwa na maradhi hayo.

Panya ni wepesi na huchukua dakika 20 pekee kukagua sampuli 100 za wagonjwa. Wanatumia hisia za kunusa na kugundua dalili za kemikali ya kifua kikuu katika sampuli.

Hilo huwafanya panya hao waliofunzwa kuwa chaguo muhimu pale muda, vifaa na pesa vinapokuwa haba katika hospitali au maabara. Wanatambua kwa usahihi visa vya TB kwa asilimia 81.



**MDUDU NYUKI**

Watafiti walifanikiwa kufunza nyuki kwa kuwapa sukari. Wadudu hawa wanaweza kugundua dalili za magonjwa fulani kupitia sampuli, ikiwa ni pamoja na saratani ya mapafu, kifua kikuu na UVIKO-19.



Wana uwezo mkubwa wa kunusa harufu ndogo sana, na hilo huwafanya kuwa na uwezo wa kugundua mabadiliko ya kemikali kama vile mbwa na panya.

Uwezo huu huwafanya nyuki kuwa muhimu kugundua magonjwa kwa njia sawa na wanyama wengine.

Ukubwa wao unaweza kuwafanya kuwa chaguo bora na la gharama nafuu kwa "uchambuzi" wa haraka wa sampuli.

**WANATAMBUAJE?**

Wana uwezo wa kugundua mabadiliko madogo katika mfumo wa harufu kupitia kemikali za mtu.

Wanatambua mabadiliko madogo katika kemikali ambayo mwili hutoa kwa viwango vya chini sana, hata wakati mtu akiwa na afya.

Pumzi ya mwanadamu inatoka takribani kemikali za gesi 3,500. Muundo na mkusanyiko wa kemikali ambazo mwili hutoa hubadilika kulingana na afya ya mtu na kemikali hizo hubadilika ikiwa mwili unapigana na maambukizi au kukabiliana na tatizo la kiafya.

Uwezo wao wa kufichua magonjwa kwa usahihi unaweza kuwa njia bora, isiyovamizi, ya haraka na ya gharama nafuu ya kutambua hali fulani.

Inaweza hata kuongeza zaidi mwingiliano mzuri kati ya watu na wanyama.

Wanyama wanaotumiwa kutambua magonjwa hutumiwa na vifaa vingine vya matibabu. Lakini ikiwa mifumo ya udhibiti itaruhusu, wanyama hawa siku moja wanaweza kuwa sehemu muhimu ya utambuzi wa magonjwa.

Mfano, mbwa wa kugundua UVIKO 19, walikuwa wepesi na bei nafuu kuliko vipimo vya kawaida.

Kwa kuelewa uwezo wa wanyama, tunaweza kuboresha uchunguzi wa maabara, ingawa kutumia ujuzi wa kunusa wa wanyama kunaweza kuwa na manufaa kwetu.

Aidha, ni muhimu kukumbuka kwamba afya na ustawi wa viumbe hawa lazima pia vipewe kipaumbele.

***BBC SWAHILI***



# Maji haya hatari kwa binadamu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, ametahadharisha kuwa mabwawa ya kuhifadhia maji na tope sumu litokanalo na uchenjuaji wa madini yasipohifadhiwa vizuri yanaweza kusababisha athari kwa binadamu ikiwamo vifo.

Mhandisi Waziri, alitoa tahadhari hiyo jana jijini hapo, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafunzo na mkutano mkuu wa mwaka wa usalama wa mabwawa ulioandaliwa na Taasisi ya Chemba ya Migodi Tanzania (TCM).

"Katika mwendelezo wa kuhakikisha tunaimarisha usalama wa mabwawa ya maji na tope sumu Tanzania Chamber of Mines kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, imeandaa mafunzo ya siku tatu yatakayoshirikisha wataalamu kutoka kwa wamiliki wa migodi kwa ajili ya usalama wa mabwawa ya tope sumu (TSF).

"Wamiliki wa mabwawa makubwa ya maji, wataalamu wa mabwawa waliosajiliwa na wataalamu kutoka serikalini ambao wanahusika na usimamizi wa mabwawa ya maji na tope sumu nao watashiriki mafunzo hayo yatakayofanyika jijini Mwanza kuanzia tarehe 16 - 18 Oktoba, 2024," alisema.

Alisema, mafunzo yatajikita kwenye ubunifu wa kapeti la kuzuia maji ya tope sumu kupenya chini ya ardhi kwa ulinzi wa mazingira hususani maji chini ya ardhi na usalama wa bwawa.

"Kwa kuzingatia kuwa, mabwawa pamoja na kuwa ni miundombinu muhimu kwa ajili ya kuhifadhi maji kwa shughuli za kiuchumi na kuhifadhi tope sumu litokanalo na shughuli za uchenjuaji wa madini, yasipohifadhiwa vizuri ni hatarishi kwa mazingira, vyanzo vya maji, mali za jamii na hata kusababisha vifo," alisisitiza Katibu Mkuu huyo.

**"Kwa kuzingatia kuwa, mabwawa pamoja na kuwa ni miundombinu muhimu kwa ajili ya kuhifadhi maji kwa shughuli za kiuchumi na kuhifadhi tope sumu litokanalo na shughuli...**

Alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa wataalamu ili kuwaongezea ujuzi wa kuhakikisha mabwawa yanayoendelea kujengwa yanakuwa salama.

"Napenda kuchukua fursa hii kuwaalika wataalamu na wamiliki wa mabwawa ya maji na tope sumu, taasisi na watu binafsi wanaojishughulisha na mabwawa kujisajili kwenye mafunzo ya ubunifu wa kapeti la kuzuia maji ya tope sumu kupenya chini ya ardhi kwa ulinzi wa mazingira na usalama wa bwawa," alisema.

Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji, Wizara ya Maji, Dk. George Lugomela, alisema wamekuwa wakitoa elimu kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria, miongozo na kanuni za uchimbaji wa mabwawa ya maji na yale ya kuhifadhia tope sumu.

"Hili ni eneo muhimu sana kwani vyanzo vyetu vya maji vingi ni vya chini ya ardhi hivyo kama hatutaweka mkazo juu ni hatari kwa watu ambao wanaweza kutumia maji yenye tope sumu," alisema.

Mwenyekiti wa TCM, Philbert Rweyemamu, alisema mafunzo hayo ni mwendelezo wa yale yaliyofanyika mwaka jana ambayo yalihusisha uwekaji wa vifaa vya kufuatilia mwenendo wa usalama wa mabwawa.

"Mafunzo hayo yaliandaliwa na TCM kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na yalijenga uelewa na kuongeza ufanisi kwa washiriki kutokana na kubadilishana ujuzi kutoka kwa wataalamu na mataifa yaliyoendelea kwenye eneo linalohusu usalama wa mabwawa hali hiyo iliwezesha kuwekwa maazimio, mojawapo likiwa ni kufanya mafunzo kama hayo kwa kila mwaka," alisema



Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida, Moses Machali, akizungumza na wafanyabiashara na wakulima waliojitokeza katika mnada wa dengu, uliofanyika kwa njia ya mfumo wa mauzo kielektroniki (TMX), katika ghala la kuhifadhia mazao la Nduguti, wilayani humo, juzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Machali ashtukia 'mchezo mchafu' zao la dengu

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali, amepiga marufuku wakulima wilayani hapa kuuza dengu shambani badala yake watumie mfumo wa stakabadhi ghalani ili kuongeza kipato.

Machali alitoa amri hiyo juzi wakati wa mnada wa kwanza wa dengu uliofanyika katika ghala la mazao lililopo Nduguti kwa mfumo wa TMX ambao umeshuhudia bei kwa kilo moja ya zao hilo ikiuzwa kwa Sh. 2,003.282.

"Lengo la serikali ni kumwinua mkulima, tunaka mkulima auze dengu yake hapa, hivyo kuanzia leo napiga marufuku kwa mtu yeyote kununua na kuuza dengu shambani," alisema Machali na kuonya kuwa: "Atakayebainika atachukuliwa hatua kali."

Kwa upande wa wafanyabiashara wa zao hilo, alipiga marufuku kusafirisha usiku bila ya kuwa na kibali cha kuthibitisha kuwa wamenunulia katika ghala.

"Kuanzia leo marufuku kusafirisha dengu wakati wa usiku kwenda wilaya nyingine ikiwa hauna kibali maalumu, natoa siku saba kwa wafanyabiashara ambao walikuwa wamenunua dengu walete hapa ghalani," alisisitiza.

Aliwakumbusha wakulima wilayani hapa kuzingatia kanuni bora za kilimo ikiwa ni pamoja na kutumia mbolea kwa wingi kwa ajili ya kustawisha mazao na kupata mavuno na kukuza uchumi wao.

"Serikali ya awamu ya sita imedhamiria kuinua sekta ya kilimo nchini, hivyo ninawasihi wakulima nendeni mkajindikishe, serikali ipo kwa ajili yenu, tumieni fursa hii vizuri," alisema Machali.

# Mbarawa atoa maelekezo 10 Sera ya Uchukuzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, ameelekeza mambo 10 ya kuzingatiwa katika uhuishwaji wa Sera ya Uchukuzi ikiwamo kudhibiti uhujumu katika miundombinu ya uchukuzi kutokana na kuanza kukithiri kwa vitendo hivyo.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye kikao cha kutoa maelekezo na mwongozo wa kuhuisha Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003 ambapo uhuwishaji wake utachukua miezi 10 kukamilika, Prof. Mbarawa, alisema tatizo la uhujumu miundombinu hiyo limeanza kujitokeza kwa kasi tofauti na awali.

Alisema lengo la kuhuisha sera hiyo ni kuhakikisha sekta ya uchukuzi inakuwa ni biashara na si huduma kama ilivyozoeleka.

"Awali huduma za usafiri na usafirishaji zilizotolewa na serikali kwa asilimia kubwa na kushauri kuwa, sera itakayohuishwa ihamasishe ushiriki wa sekta binafsi hususani katika ujenzi wa miundombinu na utoaji wa huduma," alisema.

Vilevile, alitaka suala la gharama kubwa za miundombinu linaloikabili sekta hiyo liwekwe wazi na kuwekewa mikakati katika sera itakayotungwa.

"Kadhalika izingatie uandaaji wa sera ya usafiri kwa njia ya maji inayojitegemea hatua ambayo itasaidia kuchochea shughuli za uchumi wa buluu," alisema.

Prof. Mbarawa alisisitiza kuwa, sera ya uchukuzi inayoandaliwa lazima izingatie kuendeleza ujuzi ili kuwa na wataalamu wa kutosha.

"Kwa sasa tumeingia kwenye uendeshaji wa SGR, natarajia sera itakayotungwa iweke mikakati madhubuti ya upatikanaji wa ujuzi unaotakiwa katika maeneo muhimu yakiwamo ya kukarabati, kuendesha na namna ya kutunza miundombinu iliyojengwa, na utaalamu katika urejeshaji wa fedha kubwa za umma zilizotumika. Nayo ni maeneo ya kuangaliwa," alisema.

Aliongeza kuwa, sera izingatie usafiri na usafirishaji unaozingatia utunzaji wa mazingira unaoakisi 'Green Transport' na maeneo mapya yanayoibukia katika sekta hiyo.

"Katika eneo la ubunifu mfano sera inaweza kuona namna ya kuwa na mikakati mahsusi ya matengenezo ya miundombinu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kila sekta ndogo inakuwa na mifuko ya kufanya matengenezo," alisema.

Mbarawa alisisitiza kila mdau apewe nafasi ya kutoa maoni na yazingatiwe kwa lengo la kuwa na sera pana na shirikishi inayojumuisha masuala ya uchukuzi.

"Sera izingatie ongezeko la watu nchini kama fursa kuboresha sekta ya uchukuzi; kutumika kwa jiografia ya nchi kama fursa muhimu katika masuala ya uchukuzi na namna ya kutekeleza dhana ya Tanzania kuwa kitovu cha usafirishaji katika Bara la Afrika," alisema.





# Fedha ujenzi Kituo cha Afya Ilungu zadaiwa kutafunwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHILINGI milioni 200 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Ilungu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, hazijulikani zilipo hali ambayo imesababisha ujenzi huo kusimama.

Kituo hicho kilianza kujengwa na wananchi kwa kuchangishana wenyewe na kisha aliyekuwa Mwenyekiti wa Kampuni ya IPP, Hayati Dk. Reginald Mengi akachangia Sh. milioni 25 kwa ajili ya kuwaunga mkono.

Kutokana na uhitaji wa kituo hicho, serikali ilitoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo hicho lakini wananchi wa kata hiyo wanadai kuwa halmashauri iliwaingizia Sh. milioni 300 pekee ambazo zimeshafanya kazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi, Zacharia Noti, alisema walianza kujenga kituo hicho mwaka 2017 na baadaye serikali ikawaahidi kuwapatia Sh. milioni 500 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi wao.

Alisema baada ya serikali kuahidi kutoa fedha hizo waliamua kuacha kuchangishana na wakawa wanasubiri fedha hizo ziingie ili waendelee na ujenzi.

"Tuliingiziwa Sh. milioni 300 ambazo tulijengea mpaka hapa majengo yetu yalipoishia, sasa hivi ujenzi umesimama kwa sababu fedha zile zimekwisha na zingine ...hatujui zilipelekwa wapi, tunaomba serikali ituletee fedha hizo ili tumalizie ujenzi," alisema Noti.

Kenned Mwalingo ambaye ni mmoja wa wakazi wa kata hiyo alisema kutokana na kukwama kwa mradi huo wananchi wameingiwa na hofu kuwa wanaweza wakaanza kuchangishwa tena jambo ambalo alidai litaanza kuchelewesha mradi.

Hivyo, aliiomba serikali kuwapelekea fedha zilizobaki ili wamalizie kituo hicho na huduma ziendelee kutolewa kwa wananchi akidai kuwa kwa sasa wanapata huduma.

> **"Tuliingiziwa Sh. milioni 300 ambazo tulijengea mpaka hapa majengo yetu yalipoishia, sasa hivi ujenzi umesimama kwa sababu fedha zile zimekwisha na zingine hatujui ..."**

Naye Sarafina Mweso alisema kutokana na kukwama kwa mradi huo wameanza kupata hofu ya baadhi ya vifaa ambavyo serikali imevipeleka kwa ajili ya kutolea huduma kuwa vinaweza vikaharibika kabla havijaanza kutumika.

Alisema zipo mashine mbalimbali ambazo serikali imepeleka kwenye kituo hicho lakini zimehifadhiwa na hazitumiki kutokana na kutokamilika kwa majengo ambayo zinatakiwa kufungwa.

Alisema mpaka sasa ni jengo moja pekee ndilo limekamilika na linatumika lakini mengine yaliyobaki hayatumiki kutokana na kutokamilika na hivyo akaomba serikali iwasaidie kuyakamilisha.

"Tunaamini kwamba vifaa hivi visipotumika vinaweza vikaharibika au vikaisha muda wake wa matumizi kabla havijatumika na hivyo serikali ikaingia hasara ambayo haikuwa na sababu," alisema Sarafina.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera ametoa siku 14 kwa watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwenda kushughulikia malalamiko hayo ya wananchi kabla hajachukua maamuzi magumu.

Alisema baada ya siku 14 kukamilika atakwenda kujiridhisha na kuwasikiliza wananchi wa eneo hilo na kwamba endapo watendaji hao watakuwa hawajashughulikia kero hiyo atawachukulia hatua kali.

Alisema wananchi wanachokitaka ni kupata huduma kutoka serikalini na kwamba kazi ya halmashauri ni kupeleka huduma kwa wananchi hao na hivyo akasisitiza kuwa atahakikisha kila mmoja anatimiza wajibu wake.



Meneja Uhusiano Idara ya Kilimo ya Benki ya NBC, Vivian Sakoe (mwenye kipaza sauti), akizungumza na wakulima na viongozi wa vyama vya msingi na ushirika, wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma jana, wakati wa kampeni ya 'shinda mechi zako kinamna yako na NBC Shambani' mahususi kwa wakulima wa zao la kahawa wa wilaya hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ujenzi kituo cha afya warudisha tabasamu wakazi Igalala

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

WANANCHI wa Kijiji cha Igagala Kata ya Ulembwe wilayani Wanging'ombe mkoani Njombe wanatarajia kuondokana na adha ya kusafiri zaidi ya kilometa 60 kufuata huduma za afya baada ya serikali kujenga kituo cha afya.

Walisema kituo hicho kinakwenda kuwa msaada wa kupunguza vifo kwa wajawazito na watoto ambao walikuwa wanafariki njiani kutokana na kukosa huduma za afya.

Hayo waliyasema katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, wakati akikagua ujenzi wa majengo matano ya kituo cha afya.

Majengo hayo yaliyojengwa katika eneo la Zahanati ya Igagala wilayani hapa na kutekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF). Mmoja wa wananchi hao akiwamo, Victoria Mbiduka aliiomba serikali kukamilisha kituo hicho kwa haraka ili kupata huduma za afya kwa ukaribu na kupunguza umbali mrefu wanaotumia hivi sasa.

"Ujenzi huu unaenda kutusaidia kwa kiasi kikubwa kwa sababu tulikuwa tunaenda vijiji jirani hadi wilayani ili kupata huduma lakini kikikamilika tutapata huduma zote hapa hapa hadi upasuaji," alisema Mbiduka.

Naye Erasmo Kiyule alisema licha ya uwepo wa Zahanati ya Kijiji Igaga lakini baadhi ya huduma zikiwamo za upasuaji zimekuwa tatizo kwani wajawazito wanalazimika kuwahi kwenda kusubiria kujifungua katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa au Hospitali ya Consolatha Ikonda wilayani Makete.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Igagala, Isdory Sambula, alisema tangu mradi huo ulipoanza kutekelezwa wananchi waliungana kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwamo kuchimba mawe.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Wanging'ombe, Joyce Mndemwa, alisema wameongeza majengo matano katika zahanati ya kijiji hicho kwa Sh. milioni 463 na kuahidi kukamilika ifikapo Agosti 30 mwaka huu.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Dk. Frank Chiduo alisema tayari wameandaa vifaa tiba na watumishi kwa ajili ya kituo hicho wakati wakisubiri ujenzi kukamilika.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alipongeza maendeleo ya mradi huo na kuagiza kwamba miradi yote ya ujenzi iliyopo katika mkoa huu ikamilike kwa wakati ili wananchi waanze kupata huduma.

Mtaka alisema maeneo yote ambayo kumejengwa miradi ya serikali yapimwe na hati zipatikane ili kuondoa migogoro na watu ambao wamekuwa wakivamia maeneo hayo.

# Hekari 52,000 zatengwa kwa ajili ya kilimo cha mazao

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, imetenga mashamba ya hekari 52,000 kwa ajili ya kilimo cha pamoja cha mazao mbalimbali yakiwamo ya biashara kwa lengo la kuongeza uzalishaji.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Paul Rugodisha, aliyasema hayo juzi kwenye kikao cha watendaji wa halmashauri hiyo cha kutathmini maonesho ya wakulima (Nanenane) yaliyohitimishwa Agosti 8 mwaka huu.

Alisema mashamba hayo yametengwa katika vijiji vya Nkung'ungu, Lualaje na Mapogoro wilayani humo ambavyo vina maeneo mengi yanayofaa kwa kilimo.

Alisema walitenga mashamba hayo baada ya serikali kuanzisha mpango wa kuwawezesha wanawake na vijana kupitia programu ya BBT ambapo Wilaya ya Chunya ni miongoni mwa wilaya zitakazonufaika.

Alisema halmashauri hiyo inashirikiana na Wizara ya Kilimo kuyaandaa mashamba hayo kwa ajili ya kuwagawia wakulima ambao watazalisha mazao mbalimbali.

"Tumeanza na Shamba la Kijiji cha Mapogoro ambalo lina ekari 27,000, tayari limeshakatiwa hatimiliki ambayo ni ya pamoja kati ya halmashauri yetu na wizara na tayari afya ya udongo imeshapimwa, sasa tunasubiri kuanza kuwapatia wakulima," alisema Rugodisha.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mratibu Mwandamizi wa Uhamiaji, Mbaraka Batenga, aliwataka wawekezaji mbalimbali kwenda kuwekeza kwenye kilimo katika wilaya hiyo akidai kuwa wameweandalia mazingira mazuri ya uwekezaji.

Alisema hali ya hewa ya wilaya hiyo inaruhusu kuzalisha mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula na biashara na hivyo akawataka wawekezaji hao kwenda kuwekeza.

Alisema wilaya hiyo ni miongoni mwa wilaya zinazoongoza kwa uzalishaji wa tumbaku akidai kuwa inashika nafasi ya tatu hali ambayo imeifanya kuunda mkoa wa kitumbaku.

Alisema mbali na kilimo pia wilaya hiyo inazalisha dhahabu kwa kiasi kikubwa na hivyo akawataka wawekezaji wanaotaka kuwekeza kwenye uchimbaji waende kuwekeza.

# Hospitali, vituo vya afya kuunganishwa kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuunganisha mfumo wa usajili wa kielektroniki kwa baadhi ya hospitali na vituo vya afya, ambavyo havijafikiwa na mfumo huo.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Usajili Afrika yaliyokuwa na kauli mbiu isemayo 'Kuunganisha mifumo ya usajili wa matukio ya kijamii na mifumo ya utambuzi wa watu ni muhimu kwa uchumi shirikishi'.

Alisema hatua hiyo itafanyika ili kila mwananchi aweze kupata haki ya kutambuliwa kwa kusajiliwa na kupata cheti cha kuzaliwa mara tu baada ya kuzaliwa.

Alisema serikali katika kuhakikisha hilo, imeanza kuimarisha mifumo ya usajili wa matukio ya kijamii na kuunda ofisi inayohusika na mambo hayo ikiwa na jukumu la kusajili, kuhifadhi kumbukumbu na kutoa vyeti vinavyotokana na usajili wa matukio ya kijamii.

Aidha, alisema serikali itaendelea na programu za uhamasishaji kwa wananchi juu ya umuhimu wa usajili wa matukio ya kijamii sambamba na kuweka huduma hizo karibu na maeneo ya wananchi.

"Nitumie fursa hii kuipongeza ofisi hii kwa kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yaliyowezesha usajili na uhifadhi wa matukio ya kijamii kufanya kidijitali, hatua ambayo imeleta mafanikio makubwa yenye ufanisi zaidi", alisema.

Alisema vizazi hai 90,135 vimesajiliwa katika kipindi cha kuanzia Julai mwaka 2023 hadi Juni 2024 na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa na kuongeza kuwa serikali inafurahishwa na hatua inayochukuliwa na taasisi hiyo na juhudi inazofanya kuwafikia wananchi wao.

Alisema mafanikio ambayo wameyapata yasingepatikana bila ya kuwashirikisha wananchi na kuwataka waendelee kuchapa kazi, huku maombi ambayo wameyaomba watayafanyia kazi.

Pia, aliwataka viongozi wa kisiasa kutumia ujuzi na uwezo wao katika kuwasimamia wananchi na kuwahamasisha kutumia utaratibu wa kisheria katika kufuatilia usajili wa matukio yao ikiwamo kitambulisho cha Uzanzibari ukaazi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalumu wa SMZ, Masoud Ali Mohamed, alisema usajili wa matukio una umuhimu mkubwa katika ustawi wa maendeleo ya nchi.

Hivyo, alisema bila ya usajili, suala la maendeleo kwa nchi yoyote duniani litakuwa gumu na kuwataka watendaji kuona kwamba wanayoyafanya watanguliza maslahi ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA), Mohamed Ame Makame, aliitaka serikali kufanya utaratibu wa kuimarisha huduma za mawasiliano kwa maeneo ambayo yana huduma duni za mawasiliano lakini yana idadi kubwa ya watu.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), Dk. Azzah Nofly, alisema wamepiga hatua kubwa katika safari yao ya kuunganisha mifumo katika vituo 18 vya Zanzibar' vikiwemo vinne vya binafsi kwa lengo la kutaka kuona wananchi wanapata haki zao.

# Dk. Mwinyi awashangaa wapinzani kutotaja maendeleo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema anashangazwa na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa hasa wa upinzani kutoeleza mafaniko ya maendeleo yaliyopo nchini.

Alisema hayo juzi wakati akizungumza na kamati za siasa kuanzia ngazi ya tawi, wadi, jimbo hadi mkoa katika Mkoa wa Magharibi, kichama ikiwa anakamilisha ziara zake ya kichama katika mikoa 4 ya Unguja.

Alisema yapo maendeleo makubwa yamefanyika nchini ikiwamo ujenzi wa hospitali za kisasa, shule za ghorofa, ujenzi wa nyumba za makaa na barabara, miundombinu ya maji safi na salama, lakini wapinzani wake wanapopanda katika majukwaa hawayasemi hayo kwa wananchi.

Rais Mwinyi alisema mbali na maendeleo hayo yaliyotekelezwa katika ilani kupitia sekta ya afya. Pia, serikali inakusudia kujenga upya Hospitali ya Mnazi mmoja pamoja na Binguni ambapo zikikamilika hospitali hizo wagonjwa hawatakwenda nje ya nchi kufuata matibabu.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa barabara alisema, serikali inakusudia kujenga Barabara ya Kijiji cha Mndoo hadi Miwani ambayo ni ya muda mrefu na wananchi wamekuwa wakiilalamikia kutokana na kuwa chakavu.

> **Kuhusu daftari la wapigakura, Dk. Mwinyi aliziitaka kamati za siasa kuhakikisha wanajipanga kwa ajili ya kuwaandikisha wanachama wenye sifa pamoja na kuhamasishana ...**

Kuhusu daftari la wapigakura, Dk. Mwinyi aliziitaka kamati za siasa kuhakikisha wanajipanga kwa ajili ya kuwaandikisha wanachama wenye sifa pamoja na kuhamasishana kupiga kura wakati wa uchaguzi.

Aidha, aliwataka viongozi na wanachama wa CCM kuwa na umoja na mshikamano ndani ya chama ili kutimiza adhma yao ya kushinda kwa asilimia kubwa na kuondoa manung'uniko kwa vyama vya upinzani kwa kudai kuwa wanaibiwa kura.

Kaimu Katibu wa CCM Mkoa wa Magharibi, Ali Yussuf alisema mkoa huo umeshika nafasi ya tatu kitaifa kutokana na kusajili wanachama wengi kwa mfumo wa kieletroniki na kwa upande wa Zanzibar umeshika nafasi ya kwanza.

Alisema hali ya kisiasa katika mkoa ni nzuri lakini kwa upande wa majimbo wapo baadhi ya viongozi hawashirikiani katika kazi, hali inayopelekea kuwagawa wanachama majimboni.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Magharibi, Muhammed Rajab Sudi, alisema maendeleo yaliyofanywa na Rais Mwinyi kwa miaka mitatu ni kama ya miaka 50.

Naibu Katibu Mkuu CCM Zanzibar, Dk Muhammed Said Dimwa, aliwataka wana CCM kuendelea kuhubiri umoja na kuondoa tofauti zao katika chama.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na wajumbe wa Taasisi za Benki zisizo na Mipaka ya Uingereza, ukiongozwa na Mkuu wa Taasisi hiyo, Matteo Scalabrinno (kulia kwa Rais), akiwa na ujumbe wake, Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# UN yataja dawa kumaliza vitendo vya udhalilishaji, ukatili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UMOJA wa Mataifa (UN) umesema ni vyema kukatengenezwa utaratibu kwa jamii kuzungumza katika kuzuia na kutokomeza vitendo vya udhalilishaji na ukatili.

Hayo amesema Ofisa Mradi wa kutokomeza ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto kutoka Shirika la Kimatifa la UN Women, Lucy Tesha, wakati akizungumza na wanafunzi wa Chuo cha Ufundi Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja.

Lucy alikuwa akitoa elimu ya masuala ya udhalilishaji, alisema bado kuna kundi kubwa la wanajamii hasa wasichana na watoto ambao wanapofanyiwa vitendo vya ukatili na udhalilishi huficha taarifa zao kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema wapo ambao baadhi yao watoto na wasichana hupewa vitisho endapo watatoa taarifa baada ya kufanyiwa vitendo hivyo na kukosa uthubutu wa kuripoti kutokana na hofu na woga.

Aidha, alisema lengo la kutoa mafunzo hayo kwa wanafunzi wa vyuo vya ufundi ni kutengeneza utaratibu wa jamii kuzungumza katika kuzuia ukatili na udhalilishaji wa watoto kwa sababu wanafunzi hao ni kundi kubwa ambalo likitoka kujifunza vyuoni huenda katika ajira.

Alisema katika ajira, kuna ukatili na udhalilishaji wa aina mbalimbali hivyo ni vyema wakajiandaa katika kuzuia na kutokomeza ukatili na udhalilishaji.

Ofisa Mipango wa Mamlaka ya Vyuo vya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Yahya Rashid Abdul alisema baada ya mafunzo hayo wanatarajia kutoa elimu ya udhalilishaji kwa jamii wakiwamo waendesha bodaboda pamoja na madereva na makondakta wa daladala.

Alisema bado kuna changamoto ya muhali kwa wanajamii na kukataa kutoa ushahidi kwa kesi za udhalilishaji wa kijinsia hali ambayo watuhumiwa wa matukio hayo wanashindwa kutiwa hatiani.

Mlezi wa bweni katika chuo hicho, Rajab Bahorea alisema elimu hiyo ni muhimu kwa wanafunzi ili kuepukana na vishawishi vinavyopelekea kufanya au kufanyiwa udhalilishaji. Baadhi ya wanafunzi walisema ni vyema elimu hiyo ikatolewa mara kwa mara ili kuongeza uelewa lakini pia walitaka hatua kali zichukuliwe kwa wafanyaji wa vitendo hivyo ili kuwa fundisho kwa wengine wenye tabia hiyo.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SYLIVESTA MICHAEL KIRWANDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha darasa la saba chenye index namba: **PS1404033-036** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SHULE YA MSINGI YA KIGAMBONI** mwaka 2017. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MAF/REF:9910838343198.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**GEORGE JUMA MUSA** anatangaza kupotea kwa cheti cha darasa la saba chenye index namba **PS0304088/0010** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia S**HULE YA MSINGI YA MSAGALI** mwaka 2018 na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1650/0081** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia ***SHULE YA SEKONDARI CHUNYU*** mwaka 2022. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/170080/2024, PHQ/DAR/UBU/170070/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EMMANUEL ELLY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1011/0088** Kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **CHANG'OMBE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2001 . Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **OB/RB/4424/2007**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**JUNETHER CUTHBERT PEMBA**
anatangaza kupotea kwa kadi zake za pikipiki zenye namba za usajili kama ifuatavyo:-
**MC 284 BUL** ainaya **TVS** yenye chassis namba **MD625AF43H1G88667**
**MC 291 BUL** ainaya **TVS** yenye chassis namba **MD625AF46H1G88694**
**MC 292 BUL** ainaya **TVS** yenye chassis namba MD625AF42H1G88692
MC 394 BUL ainaya TVS yenye chassis namba **MD625AF48H1G88678**
Kwa yeyote atakayeziona anaombwa kutoa taarifa kituo chochote cha Polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/TAN/TAN/6212/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**JUNETHER CUTHBERT PEMBA**
anatangaza kupotea kwa kadi zake za pikipiki zenye namba za usajili kama ifuatavyo:-
**MC 577 BJH** aina ya **TVS** yenye chassis namba **MD625AF42G1A68679**
**MC 926 BNG** aina ya **TVS** yenye chassis namba **MD625AF48G1K20428**
**MC 277 BUL** aina ya **TVS** yenye chassis namba **MD625AF45H1G88685**
Kwa yeyote atakayeziona anaombwa kutoa taarifa kituo chochote cha Polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/TAN/TAN/6212/2024**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA SONGEA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBI NAMBA 73/2024**

**SKINAI RASHID CHOWO –––––– MLETA MAOMBI**

**(Msimamizi wa mirathi ya marehemu, Rashidi Swalehe Chowo)**

**DHID YA**

**ALLI TWAIBU KATAWALE}**
**SHAIBU SALEHE KATAWALE } –––WAJIBU MAOMBI**

**WITO /KUITWA SHAURINI .**

Alli Twaibu Katawale unataarifiwa kuwa Mleta Maombi amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako .Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au Wakili wako ,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 27/08/2024 saa 3:30 asubuhi.Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwaajili ya kuleta hati zako za utetezi.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wako.

Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 05/08/2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SONGEA

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF RUNGWE DISTRICT AT TUKUYU**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 19171/2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GERALD JAPHET URASSA**

**AND**

**ATUGANILE ASAFYISYE MWANGOSI......PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 02nd day of SEPTEMBER,

Dated at Rungwe this 09th day of AUGUST 2024.

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
RUNGWE - TUKUYU

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 19547 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late CHRISTINA ONESMO MTWALE of Dodoma**

**Within Dodoma City.**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY CHIPEGWA TITO CHIWELESA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 04 Day of 09, 2024
Dated at Dodoma this 13 Day of 8, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 18744 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late: LUCY AWARD MWAMSOJO**

**By 1: GODFREY STEPHEN KUSILA**
**2: ______________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 29 day of August.2024

Dated at Morogoro this 13 day of August.2024

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O.Box 660, Morogoro

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA




Polisi akiwa na mwamvuli kwa ajili ya kujizuia na jua kali wakati akiongoza vyombo vya usafiri katika barabara moja katika jiji la Dhakar nchini Bangladesh juzi. **PICHA: AFP**

# Watanzania bado wako salama, udhibiti wa Mpox umechukuliwa

**Na Moshi Lusonzo**

WIZARA ya Afya imesema kuwa imechukua hatua madhubuti kukabili ugonjwa wa homa ya nyani, unaojulikana kama MPox, baada ya Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa barani Afrika (CDC), kuutangaza kuwa dharura ya kiafya kwa umma.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Ofisa Habari wa Wizara ya Afya, Englebert Kayombo, alisema ni vizuri Watanzania kuondoa hofu na kuchukua hatua za kiafya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.

Alisema wameipata taarifa hiyo ya CDC na kama nchi tayari imeimarisha na kuboresha mifumo ya kudhibiti mlipuko wa ugonjwa huo.

"Tumepata taarifa ya kutangazwa kwa tahadhari ya janga la ugonjwa huo, inamaanisha tumechukua juhudi za makusudi kama Tanzania kuonesha mifumo yetu ya kudhibiti ugonjwa huu" alisema Kayombo.

Alisema mpaka sasa hakuna kisa kilichoripotiwa cha mtu kuwa na ugonjwa huo na kwamba wamechukua hatua mbalimbali za tahadhari kwa kuboresha huduma ya uchunguzi kwenye mipaka na njia zote za usafirishaji.

"Tumeboresha huduma ya uchunguzi kwa watu wanaoingia nchini kupitia mipakani na viwanja vya ndege, huko kuna maofisa wa afya wanaofanya vipimo kubaini watu wenye dalili za ugonjwa huo na kama watapatikana watawahishwa hospitalini," alieleza.

Aidha, alisema serikali inaendelea kutoa elimu kwa raia wa kada zote kuhakikisha wanaepuka kugusana na watu wenye dalili za homa ya nyani.



Alisisitiza kwamba endapo kwa bahati mbaya ugonjwa huo ukaingia nchini, hospitali zina uwezo wa kutoa tiba za ugonjwa huo haraka.

Juzi, Mwenyekiti wa CDC yenye makao makuu yake nchini Ethiopia, Jean Kasenya, alisema usambaaji wa ugonjwa huo umefikia kiwango cha juu, hivyo aliutaja kama ugonjwa wa dharura na kutahadharisha nchi mbalimbali kuchukua hatua ya kuzuia.

Alisema jumla ya visa 38,465 vya ugonjwa huu vimerekodiwa katika nchi 16 za Afrika tangu mwezi Januari 2022, huku vifo vilivyoripotiwa ni 1,456.

Kulingana na data zilizochapishwa wiki iliyopita na kituo hicho, kuna ongezeko la asimilia ya maambukizi ndani ya mwaka huu ikilinganishwa na mwaka uliopita

„Mlipuko wa Mpox sasa umevuka mipaka, na kuathiri maelfu ya watu katika bara letu. Ninaamua kusema kwa moyo mzito lakini kwa dhamira isiyotetereka kwa raia wetu wa Kiafrika, kwamba tunatangaza mlipuko wa Mpox kama dharura ya afya ya jamii barani Afrika," alisema Kasenya.

Aliongeza „Tamko hili si jambo la kawaida tu, ni wito wa wazi wa kuchukua hatua. Ni utambuzi ambao hatuwezi kuumudu tena kuwa watendaji. Ni lazima tuwe watendaji na majasiri katika juhudi zetu za kudhibiti na kumaliza janga hili,"

Tangazo hilo litafanya uwezekano wa kutoa fedha kwa ajili ya kununua chanjo na kutarajia mwitikio katika nchi za Kiafrika kupambana na ugonjwa huo.

Katika mkesha wa mkutano wa kamati ya dharura ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ulifanya mkutano wiki iliyopita kwa ajili ya kutathmini ikiwa kuna umuhimu wa kutangaza kiwango cha juu cha tahadhari ya afya katika ngazi ya kimataifa dhidi ya ugonjwa huo.

Afrika inakabiliwa na kuenea kwa aina mpya ya virusi hivyo, iliyogunduliwa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) mnamo mwezi Septemba 2023 na kuitwa „Clade Ib", ambao ni hatari zaidi na inayoambukiza zaidi kuliko ile yaliyotangulia.

Kesi za kuenea kwa Mpox, zimerekodiwa katika mataifa mbalimbali ya Afrika ikiwamo Morocco, Misri, Sudan, Ivory Coast, Liberia, Nigeria, DRC, Rwanda, Kenya, Msumbiji na Afrika Kusini.

Kulingana na CDC, kiwango cha vifo vinavyotokana na virusi ni zaidi ya asilimia 3 ya wagonjwa, watoto chini ya miaka 15 ndio walioathirika zaidi, ikichukua asilimia 60 ya kesi zote.

Mpox ni ugonjwa unaoambukizwa kutoka kwa wanyama hadi kwa binadamu kwa njia ya kugusana kwa karibu na mtu aliyeambukizwa virusi.

Clade Ib husababisha vipele kuonekana kwenye mwili wote, ambapo aina za awali zilikuwa na upele na vidonda kwenye mdomo, uso au sehemu za siri.

Mpox iligunduliwa kwa mara ya kwanza kwa binadamu mnamo mwaka 1970 katika nchi ambayo sasa inaitwa DRC (zamani Zaire), na kuenea kwa aina ndogo ya Clade.

## Marekani yaiuzia Israel zana za kijeshi

**WASHINGTON,** MAREKANI

SERIKALI ya Marekani imeidhinisha uuzaji wa ndege za kivita zenye thamani ya dola bilioni 20 na vifaa vingine vya kijeshi kwa Israel.

Israel inaendeleza vita vyake vya miezi 10 katika Ukanda wa Gaza dhidi ya kundi la Hamas.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken ameidhinisha uuzaji wa takriban dola bilioni 19 za ndege na vifaa vya F-15, pamoja na risasi za mizinga zenye thamani ya dola milioni 774.

Pia katika mauzo hayo zaidi ya dola milioni 60 kwa ajili ya vilipuzi na magari ya kijeshi yenye thamani ya dola milioni 583.

"Marekani imejitolea kwa usalama wa Israel na ni muhimu kwa maslahi ya kitaifa ya Marekani kusaidia Israel kuendeleza na kudumisha uwezo imara, tayari kwa ulinzi."

Ilisema taarifa ya wizara hiyo.Katika chapisho kwenye mtandao wa X, Waziri wa Ulinzi wa Israel Yoav Galant, aliwashukuru maofisa wa Marekani kwa kuisaidia Israel kudumisha makali yake ya kijeshi katika eneo hilo na kujitolea kwa Marekani kwa usalama wa nchi yake.

Rais wa Marekani Joe Biden, alisema kuwa kufikiwa kwa makubaliano ya kusitisha mapigano kati ya Israel na Hamas huko Gaza kunaweza kusaidia kuizuia Iran kufanya mashambulizi dhidi ya Israel.

„Tutaona Iran itafanya nini na nini kitatokea ikiwa kutakuwa na shambulio, lakini sitakata tamaa," alisema Biden wakati akishuka kutoka kwenye ndege yake wakati wa ziara ya New Orleans, Louisiana.

Hofu kuhusu kulipiza kisasi kwa Iran bado imeendelea kuwepo baada ya mauaji ya mkuu wa kisiasa wa Hamas Ismail Haniyeh, yaliyofanyika mjini Tehran Julai mwaka huu, ambayo Israel haijadai kuhusika nayo.

Kwa upande wake balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa amesema kuwa, nchi yake inalenga kudhoofisha wasiwasi katika eneo la Mashariki ya Kati kuhusu ulipaji kisasi kwa Iran.

**BBC**

# SERIKALI YASIKIA KILIO CHA WAOGELEAJI

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya maombi ya muda mrefu ya waogeleaji na Chama cha mchezo huo Tanzania (TSA) ya kutaka kujengewa Bwawa kubwa la kisasa kwa ajili ya mazoezi na mashindano, hatimaye serikali imeanza ujenzi wa bwawa la mita 50 nyuma ya Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Michezo wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Charles Maguzu alisema bwawa hilo litakuwa na ubora wa hali ya juu kwani malengo ni kuona Tanzania inafanya vizuri katika mchezo wa kuogelea katika mashindano mbalimbali.

„Serikali tayari imeanza ujenzi wa bwawa la kisasa la mita 50 ambalo litakidhi vigezo vya Olimpiki ambalo litawasaidia waogeleaji kujiandaa na michezo hiyo ya mwaka 2028,“ alisema Maguzu.

Ofisa huyo aliwataka wachezaji wote waliokuwa wamekwenda kushiriki Olimpiki nchini Ufaransa katika Jiji la Paris wasikatishwe tamaa na matokeo waliyoyapata bali wajipange kwa ajili ya mashindano yajayo.

Alisema wataendelea kushirikiana na Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC) katika maandalizi ya kuandaa timu ambazo zitakwenda kushiriki michezo hiyo ya mwaka 2028.

Kwa upande wake Kocha Mkuu wa timu ya taifa ya kuogelea, Alexander Mwaipasi alisema anaipongeza serikali kwa kuamua kujenga bwawa hilo ambalo litasaidia kuinua vipaji vya waogeleaji nchini.

„Waogeleaji wamekuwa wakifanya mazoezi katika mazingira magumu kwa kuwa hatuna bwawa lolote zaidi ya kutegemea mabwawa ya shule za watu binafsi, hivyo tunaishukuru serikali kwa maamuzi hayo, alisema Mwaipasi.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Lumumba jijini Dar es Salaam, wakifanya mazoezi ya kucheza mpira wa magongo katika Uwanja wa Jakaya Kikwete, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Watalii, Wakimbiza baiskeli kusaka Panya masikio marefu Kilimanjaro

**Na Mary Mosha, MOSHI**

WATALII zaidi ya 1000 kutoka mataifa mbalimbali watashiriki mbio za baiskeli pamoja na zoezi la kuwasaka na kuwaona panya wenye masikio yanayofanana na masikio ya tembo kwenye msitu wa Rau, uliopo Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro .

Tukio hilo lililopewa jina la ‚tukacharo Rau‘ ambalo linalenga kufanya shughuli za utalii kwenye msitu huo, litaenda sambamba na mbio za baiskeli na utalii wa kutembea peku ndani ya msitu.

Akizundua msimu wa pili wa ‚Tukacharo Rau“ Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Zephania Sumaye alisema lengo la TUKACHARO ni kutangaza utalii wa ndani ya Manispaa ya Moshi na mkoa kwa ujumla.

Alisema watakaoshiriki wataweza kuwaona panya wenye masikio yaliyofanana na yale ya tembo, hali ya hewa inayoridhisha licha ya kuwepo katikati ya mji, Mbega weupe na mti mkubwa kuliko yote barani Afrika (Mvule).

**“Msitu huu upo ndani ya mji wa moshi lakini unapokuwa humu ndani unaweza usitambue kama upo mjini Moshi, huku tuna maeneo ya kupumzika, kufanya mila ya tamaduni, kutembea kwa ukimya (wengine hutumia kama eneo la ibada),“alisema Sumaye. Alisema siku hiyo kutakuwa ni ‚Bush Party‘, vyakula vinywaji huku wakiwakaribisha wadhamini kuunga mkono kwa kudhamini tamasha hilo.**

Naye Mhifadhi Mkuu wa misitu wilaya ya Moshi, Godson Ulomi, alisema kutakuwa na kukimbia na kuendesha baiskeli kilomita 75.

“Tunawakaribisha katika ‚TUKACHARO msimu wa pili, msimu wa kwanza tulikuwa na washiriki zaidi 300 na baada ya zoezi lile, utalii umezidi kuongezeka sana, kwa msimu huu tumeboresha zaidi na hadi sasa tayari wameshajiandikisha zaidi ya watu 300 na tunatarajia zaidi ya watu 1000,“ alisema Ulomi.

# Kocha Tenisi ahaidi ubingwa wa Vijana

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA wa timu ya taifa ya vijana ya mchezo wa tenisi, Majuto Majaliwa, ameahidi kutwaa ubingwa kwenye mashindano ya vijana wenye umri chini ya miaka 12 ya Ukanda wa Afrika Mashariki yanayoendelea kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Majaliwa alisema katika mashindano hayo, timu itakayofanya vizuri itapata nafasi ya kwenda kushiriki mashindano ya vijana ya Afrika yatakayofanyika mwezi Septemba nchini Misri.

„Kwa upande wetu tumejipanga vizuri kuhakikisha tunaibuka na ubingwa katika mashindano haya kutokana na uwapo wa wachezaji wengi wachanga na wenye vipaji,“ alisema Majaliwa.

Alisema kwa maadalizi yao, wanauhakika wa kuchukua ubingwa huo na kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya vijana ya mwezi Septemba.

Aidha, aliwataka wadau mbalimbali wa mchezo huo wawaunge mkono ili watimize malengo waliyojiwekea kuhakikisha ubingwa huo unabaki nyumbani.

Kwa upande wake, Ofisa kutoka Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Ingridi Kimario, alipongeza viongozi pamoja na wadhamini wa mashindano hayo kutokana na juhudi wanazoendelea kuzifanya kuhakikisha mchezo huo unazidi kukua.

Alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi nane ambapo alizitaja baadhi ya nchi hizo kuwa ni Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Somalia, Djibuti, Sudan pamoja na wenyeji Tanzania. Wakati huo huo Makamu wa Rais wa Chama cha Michezo wa Tenesi Tanzania (TTA), Rajab Boli alisema amefurahi kuona Tanzania imepata nafasi ya kuandaa mashindano hayo.

Aidha, aliishukuru BMT kwa kushirikiana na uongozi wa Klabu ya Gymkhana kwa kuwapa kibali cha kuendesha michuano hiyo.

## ZISIKUPITE

### BRENTFORD IMESHIKILIA PALEPALE

BRENTFORD inashikilia kuwa pauni milioni 60 ndio gharama ya kumuuza mshambuliaji wa England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 28 ambaye anafuatiliwa na Chelsea na Manchester United. ***(Independent)***

### AJAX INAVUTIWA ZAIDI NA RAMSDALE

KLABU ya Ajax ina nia ya kumsajili kipa wa Arsenal, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 26. ***(Sky Sports).***

### VINICIUS JR HATARUHUSIWA KUONDOKA

REAL Madrid haitamruhusu mshambuliaji wa Brazil, Vinicius Junior mwenye umri wa miaka 24 kuondoka kwenda Saudi Arabia hata kama watapokea ada ya kuvunja rekodi ya dunia. ***(AS)***

### WAARABU WAGOMA KUMUUZA KANTE

KLABU ya Al-Ittihad haitaki kumuuza kiungo wa kati wa Ufaransa, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 33, licha ya kuhusishwa na West Ham na Atletico Madrid. ***(Fabrizio Romano)***

### NKETIAH MBADALA WA SOLANKE B'MOUTH

KLABU ya Bournemouth inamlenga mshambuliaji wa Arsenal, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 25, ili kuziba pengo la Dominic Solanke anayetarajia kuelekea Tottenham Hotspur. ***(Mail)***

### BRIGHTON YAMGANDA OLIVIER BOSCAGLI

KLABU ya Brighton ina nia ya kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Olivier Boscagli mwenye umri wa miaka 26, lakini klabu yake ya PSV Eindhoven inataka zaidi ya walichotoa Seagulls hao. ***(Eindhovens Dagblad)***

### LEICESTER CITY YAMWANIA AYEW

KLABU ya Leicester City imetoa ofa ya pauni milioni nne kwa fowadi wa Crystal Palace na Ghana, Jordan Ayew mwenye umri wa miaka 32. ***(Mail)***

### BARCA YAIWEKEA NGUMU EVERTON

BARCELONA imekataa ofa ya Everton ya pauni milioni 23.9 ikijumuisha nyongeza ya malipo kwa mshambuliaji wa Brazil, Vitor Roque mwenye umri wa miaka 19. ***(Sky Germany)***

### ALONSO KUTUA MACHESTER UNITED

KLABU ya Manchester United ina nia ya kumsajili beki wa zamani wa Chelsea na Hispania, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 33 ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Barcelona**. *(Athletic)***

### DAVIES KUMALIZA MKATABA SPURS

BEKI wa Wales, Ben Davies mwenye umri wa miaka 31, huenda akakamilisha mwaka wa mwisho wa mkataba wake na Tottenham Hotspur badala ya kutafuta uhamisho msimu huu wa joto. ***(Football Insider)***

### NAPOLI, LEIPZIG KWA OMORODION

NAPOLI na RB Leipzig zinaongoza katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid, Samu Omorodion mwenye umri wa miaka 20 baada ya uhamisho wake kwenda Chelsea kushindikana. ***(Football Insider)***

### PHILLIPS KWA MKOPO GETAFE

GETAFE ina nia ya kumchukua kwa mkopo beki wa kati wa Tottenham Hotspur, Ashley Phillips mwenye umri wa miaka 19. ***(Sky Sports)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARAUJO AJIUNGA NA BOURNEMOUTH

●●●Nyota huyo wa Mexico amejiunga na timu hiyo ya England baada ya Barcelona kukubali kupokea kiasi cha...

**LONDON, England**

MCHEZAJI wa kimataifa wa Mexico mzaliwa wa Marekani, Julian Araujo amejiunga na klabu ya Ligi Kuu ya England, Bournemouth kutoka Barcelona kwa uhamisho wa thamani ya Euro milioni 10, klabu hizo mbili zimethibitisha.

Araujo mwenye umri wa miaka 22, alijiunga na Barca kutoka LA Galaxy mwaka wa 2023 lakini hakupata nafasi katika klabu hiyo akitumia msimu uliopita kwa mkopo huko Las Palmas.

"Ni mchezaji mchanga mwenye uwezo wa hali ya juu na tumefurahi kushinda ushindani mwingi kuwania saini yake," alisema Mtendaji Mkuu wa Bournemouth, Neill Blake katika taarifa yake.

"Tunaamini kwamba tuna zana zote hapa kwa ajili ya Julian kuongeza uimara na ubora ambao tayari anao na tunatazamia sana kumkaribisha kwenye Uwanja wa Vitality," alisema Blanke.

Kocha mpya wa Barca, Hansi Flick, alimtazama Araujo kabla ya msimu mpya na kumpa dakika dhidi ya Manchester City huko Orlando.

Hata hivyo, Araujo hakuweza kupata nafasi katika mipango ya Flick ya kampeni ijayo, na kumlazimu beki huyo wa pembeni kutafuta dakika nyingi za kucheza sehemu nyingine.

Araujo, ambaye alicheza mechi zaidi ya 100 katika klabu ya MLS ya LA Galaxy, alijiunga na Barca kwa mara ya kwanza Januari 2023 lakini alitumia miezi sita ya kwanza bila kucheza kwa sababu dili hilo lilikuwa limekamilika sekunde chache baada ya dirisha la uhamisho kufungwa.

Kisha alijiunga na timu ya Laliga ya Las Palmas kwa mkopo msimu uliopita, na kucheza mechi 28 katika mashindano yote, hasa katika nafasi ya beki wa kulia.

Baada ya kuiwakilisha Marekani katika timu za vijana na hata kucheza moja ya wakubwa, beki huyo mzaliwa wa California aliamua kubadili taifa la kuchezea na kuamua kuiwakilisha Mexico mwaka 2021.

# MAN UTD KUMKOSA LUKE SHAW MAPEMA

**MANCHESTER,** ENGLAND

MANCHESTER United imefichua kwamba beki wake wa kushoto, Luke Shaw hatakuwapo mwanzoni mwa msimu mpya baada ya kupata jeraha la mguu katika mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya.

Shaw alipata tatizo la nyama za paja Februari na akakosa miezi michache ya mwisho ya kampeni ya Ligi Kuu ya 2023/24, akirejea tu katika hatua za mwisho za kampeni ya England za Euro 2024.

Beki huyo wa kushoto hakushiriki katika mechi za kirafiki za kujiandaa na msimu mpya, hata hivyo, United sasa wamethibitisha kuwa kuna tatizo jipya la kukosekana kwa Shaw.

„Luke Shaw atakosa mechi za ufunguzi wa msimu wa Ligi Kuu kwa sababu ya jeraha la mguu alilolipata mwanzoni mwa mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya," taarifa fupi ilisoma.

„Anafanya kazi kwa bidii katika kurejea kwenye hali yake ya kawaida kwa nia ya kupatikana baada ya mapumziko ya kwanza ya kimataifa."

Mapumziko ya kwanza ya kimataifa yanakuja baada ya wikiendi ya kwanza Septemba, wiki tatu za msimu mpya.

United watafungua kampeni yao msimu huu nyumbani kwa Fulham na kisha watasafiri kumenyana na Brighton & Hove Albion kabla ya ziara kubwa kutoka kwa Liverpool kuwapeleka kwenye mapumziko ya kimataifa.

Ni jinsi gani Erik ten Hag atachukua nafasi ya Shaw bado haijaonekana.

Naibu wake Tyrell Malacia hatarajiwi kurejea tena hadi Oktoba kwani anaendelea kupata nafuu kutokana na jeraha lililomfanya akosekane kwa msimu mzima uliopita, na kuiacha United bila mbadala wowote wa asili.

Beki wa kati Lisandro Martinez alianza katika upande wa kushoto kwenye kichapo cha Ngao ya Jamii kutoka kwa Manchester City, huku Ten Hag akikataa nafasi ya kumpa dakika zaidi Harry Amass mwenye miaka 17 baada ya mchezo mzuri wa kujiandaa na msimu mpya.




## Palmer ajifunga Chelsea hadi 2033

**LONDON,** ENGLAND

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa England, Cole Palmer ametia saini mkataba wa nyongeza wa miaka miwili utakaomfunga Chelsea hadi 2033, klabu hiyo ya Ligi Kuu England ilisema jana.

Palmer alijiunga kutoka Manchester City Septemba mwaka jana na alikuwa mmoja wa wachezaji bora kwenye Ligi Kuu akimaliza kampeni akiwa na mabao 22 nyuma ya Erling Haaland wa Manchester City -- na kupata nafasi katika kikosi cha England kwa mashindano ya Ulaya.

Palmer mwenye umri wa miaka 22 aliifungia England kama mchezaji wa akiba kwenye mchezo fainali ya Euro walipoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Hispania kwenye fainali.

Sasa amesajiliwa Chelsea kwa miaka tisa ijayo, akiendelea na sera ya klabu hiyo ya kuwafunga wachezaji wake chipukizi kwa mikataba ya muda mrefu.

„Nilipata mafanikio mengi katika msimu wangu wa kwanza hapa," alisema.

„Na ninatumaini ninaweza kuendelea kupata uzoefu mzuri katika klabu hii, katika ngazi ya binafsi na katika kuleta mafanikio na mataji kwa Chelsea."

Palmer yuko kwenye orodha ya wachezaji sita walioteuliwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa Chama cha Wachezaji Soka wa Kulipwa. Mshindi atatangazwa Agosti 20.

## Man City ‚yabetiwa' kubeba taji EPL au kushuka daraja

**LONDON,** ENGLAND

IKIZINGATIWA kuwa imeshinda mataji sita kati ya saba ya Ligi Kuu England, Manchester City inapewa nafasi ya juu kushinda ligi kwa mara nyingine msimu huu, kwa mujibu wa ESPN.

Manchester City wanaongoza katika wale wanaopewa nafasi ya kuwa „Mshindi wa Ligi" wakiwa na odd +120, wakifuatwa kwa karibu na Arsenal wenye +180 na kwa ukaribu kidogo na Liverpool kwa +700.

Uwezekano huo unasababisha kushuka kwa kiwango kikubwa kutoka hapo, huku Chelsea na Manchester United zikiwa zimefungana kwa odd +2200, kwa kila ESPN BET.

Watu wengi wanategemea City kushinda taji lao la tano mfululizo msimu huu, kwani wamenyakua asilimia 26 ya tiketi katika ESPN BET, asilimia 18.2 BetMGM na asilimia 50 katika DraftKings, mbili za mwisho zikiwa zinaongoza uwanjani.

Lakini ni Arsenal ambayo ipo juu ikipewa nafasi ikichukua asilimia 54 inayoongoza kwa ESPN, asilimia 37 katika DraftKings na asilimia 31 kwa FanDuel, huku Liverpool pia wakipiga kelele kwenye ESPN BET na wakiwa na asilimia 18% ya pesa.

Kinyume chake, Man City wana asilimia 8 tu katika ESPN BET.

Klabu hiyo inakadiriwa kutawala kama ilivyokuwa katika misimu kadhaa iliyopita, lakini uwezekano wake wa kushinda mechi zote umeshuka kutoka -120 kwenye uwanja wa wazi katikati ya Mei hadi nafasi yao ya sasa.

Hatua hizo na hatua ya kamari dhidi ya City ni matokeo ya mashtaka yanayosubiriwa ya udhibiti wa fedha dhidi yao, huku hukumu, ikijumuisha rufaa, ikitarajiwa kufikiwa mwishoni mwa msimu huu.

Iwapo Ligi Kuu itaipata Manchester City na hatia ya ukiukaji fulani au wowote, klabu hiyo inaweza kukabiliwa na kupunguzwa kwa pointi kwa msimu au hata kushushwa daraja.

Hiyo ina maana kwa waweka dau wa siku zijazo kuzingatia sheria za nyumbani za vitabu vya michezo.

Katika ESPN BET na vitabu vingi muhimu, ikiwa timu itashushwa daraja kutokana na kupunguzwa kwa pointi na kuiweka katika eneo la kushushwa daraja mwishoni mwa msimu, wachezaji wanaocheza dau husika katika soko la kuteremka daraja watawekwa alama kuwa washindi.

Lakini ikiwa timu itashushwa kutoka ligi na bodi inayosimamia kabla ya mwisho wa msimu, bila kujali alama, dau hizo zitachukuliwa kuwa tupu na kurejeshwa.

Kwa hivyo, wadau wengi wanamiminika kwenye soko la Manchester City la „Ili Kushushwa Daraja", wakitazamia njia ya kupunguza pointi. Katika odds +1500, klabu inaongoza kwa 27% ya dau na 45% ya mpini katika ESPN BET.

Vivyo hivyo kwa BetMGM, ambayo ina 24.2% ya tiketi zake za kushuka daraja kwa Man City kuwa dhima yake kubwa kwa soko hilo, kitabu ipasavyo kilihamisha uwezekano wa timu kushuka daraja kutoka +1600 kwa wazi hadi +1000.

# KMC YAWAITA SIMBA MEZANI KUMCHUKUA AWESU AWESU

**Na Faustine Feliciane**

SIKU moja baada ya Kamati ya Sheria na Hadhi ya Wachezaji wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kutoa maamuzi ya sakata la usajili wa kiungo Awesu Awesu aliyerudishwa kwenye klabu yake ya KMC baada ya usajili wa Simba, uongozi wa wana Kinondoni hao umesema upo tayari sasa kufanya biashara na wenzao hao.

Jana kamati hiyo ilibatilisha usajili wa Awesu kwenda Simba kutokana na kile ilichosema usajili huo haukuwa halali licha ya Simba kumtangaza mchezaji huyo na kwenda naye Misri kwenye maandalizi ya msimu.

Mwenyekiti wa KMC, Kheri Nassoro, alisema wapo tayari kukaa mezani na uongozi wa Simba kujadiliana biashara ya kuwauzia kiungo huyo.

Nassoro alisema kuwa lengo lao ni kuona mchezaji anacheza mpira kwa taratibu zilizowekwa na mamlaka na si vinginevyo.

Tunashukuru kwa maamuzi haya, tunataka kuona soka letu linafuata taratibu, tupo tayari kuzungumza na wenzetu wa Simba kuona tunafikia wapi,“ alisema Nassoro.

Alisema kuwa dirisha la usajili wa wachezaji linamalizika leo saa 5:59 hivyo leo muda upo wa kukaa pamoja na kufikia muafaka wa usajili huo.

“Hakuna haja ya kumwekea kipingamizi mchezaji, mpira ni kazi yake na sisi klabu ndiyo kazi yetu. Tunachotaka hapa ni kufuatwa kwa sheria. Viongozi wa Simba wapo na sisi tupo pia, waje mezani kwa majadiliano na endapo tutakubaliana, basi atacheza Simba na wala si vinginevyo,” alisema Nassoro.

Katika maamuzi yake yaliyotokana na kikao cha Agosti 10, Kamati hiyo ilibaini ukiukwaji wa taratibu za usajili wa mchezaji huyo na kuamuru kurejea klabu yake ya zamani.

Kamati hiyo ilisikiliza pande zote mbili (KMC FC na Simba SC), na kuamua kuwa Awesu ni mchezaji halali wa KMC FC, na kama Simba SC inamwitaji izungumze na klabu yake.

Kamati hiyo ilisema kuwa haikupata ushahidi wowote kutoka kwa KMC kuwa Simba SC ilimrubuni mchezaji huyo kwenda Simba lakini wameipa klabu hiyo na kusisitiza ifuate taratibu pale inapohitaji kusajili mchezaji.



Vijana wanaolelewa katika Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam, wakiwania mpira walipokuwa wakifanya mazoezi katika uwanja wa kituo hicho jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Coastal yaifuata Bravos ikifunga usajili na watatu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Coastal Union kikiondoka alfajiri ya kuamkia jana kuelekea Angola kwa ajili ya mchezo wa awali wa Kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi ya Bravos do Maquis utakaochezwa Jumamosi ijayo, uongozi wa timu hiyo umewatangaza wachezaji wapya watatu ambao wamefunga usajili kwa msimu huu.

Klabu hiyo imewatangaza mshambuliaji Maulidi Shaaban na beki wa kulia Aidan Rasmos, wote kutoka Mbeya City na winga wa kushoto, Jeremie Ntambwe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo inasema kuwa wachezaji hao watatu ndiyo wanaofunga usajili kwa msimu huu na wanaimani kuwa kikosi sasa kimekamilika kwa ajili ya michuano ya kimataifa na Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo msimu ujao imejipanga kumaliza nafasi ya juu zaidi ikishindikana watetee nafasi yao ya nne waliyomaliza msimu uliopita.

Usajili wa wachezaji kwa madaraja yote nchini unatarajia kukamilika leo saa 5:59 usiku, huku Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), likionya kuwa hakutakuwa na muda wa ziada.

Kabla ya kuwasainisha wachezaji hao, tayari Coastal ilikuwa imewasajili wachezaji wengine wapya ambao ni Henest Malonga, John Makwata, Banza Kalumba, Athumani Msekeni, Haroub Mohamed, Mukrim Issa, Ramadhani Mwenda, Abdallah Hassan na Anguti Luis.

Wakati uongozi ukikamilisha usajili huo, tayari kikosi cha timu hiyo kipo nchini Angola kwa ajili ya mechi yao ya Jumamosi ijayo dhidi ya Bravos do Maquis.

Meneja wa timu hiyo, Yassin Napili alisema kikosi chao kipo vizuri kwa ajili ya mchezo huo huku akikiri kuwa kuna makosa madogo madogo ambayo Kocha Mkuu, Mkenya, David Ouma ameyaona na atayarekebisha kabla ya mechi hiyo.

Coastal Union imepata nafasi ya kushiriki michezo ya kimataifa kwa mara ya kwanza baada ya miaka 35 kwa kuwa ilifanikiwa kumaliza katika nafasi na nne kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita.

Mara ya mwisho kwa Coastal kucheza michezo ya kimataifa ilikuwa mwaka 1989 baada ya kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara.

## Gamondi apania kumaliza kazi mchezo wa kwanza

INATOKA UK. 24

yake ya ushambuliaji, ambapo katika michezo sita waliyocheza tangu wakiwa Afrika Kusini ilipocheza mechi tatu, na miwili ya Ngao ya Jamii ikiwa hapa nchini, imefunga mabao 13, na kuruhusu manne, ambapo katika michezo hiyo sita, wameshinda michezo mitano na kupoteza mchezo mmoja.

Ilianza kwa kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya Augsburg, ikaifunga TS Galaxy bao 1-0, na baadaye ikaikandika Kaizer Chiefs mabao 4-0.

Iliporejea nchini ilicheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Red Arrows ya Zambia, kilele cha Wiki ya Mwananchi na kushinda mabao 2-1, ikaichapa Simba bao 1-0 kabla ya kuichakaza Azam mabao 4-1 kwenye hatua ya nusu fainali na fainali ya Ngao ya Jamii.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, akizungumza na Nipashe jana, alisema wamejipanga hasa katika mchezo huo wa kwanza.

“Tumejiandaa vyema, wanachama na mashabiki wa Yanga watuombee dua tushinde mechi ya kwanza mabao mengi, tukishinda hivyo basi mechi ya marudiano ambayo kikanuni tutakuwa tunacheza nyumbani tunakwenda tu kumalizia malizia kazi, maana kwetu itakuwa kama mtoko tu,“ alisema Kamwe.

Mechi ya Jumamosi itakayochezwa, Uwanja wa Azam Complex, kikanuni Yanga itakuwa mgeni dhidi ya timu hiyo ya Burundi ambayo imeamua kuhamishia michezo yao hapa nchini.

Baada ya mchezo huo, Yanga itarudia na Vital'O, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaaam, Agosti 24, mshindi wa jumla kati ya timu hizo mbili atacheza na mshindi kati ya CBE ya Ethiopia au SC Villa ya Uganda katika hatua ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Fadlu awashusha presha mashabiki

INATOKA UK. 24

ya mashabiki wa timu hiyo ambao wamekosa ubingwa wa Ligi kwa misimu mitatu mfululizo.

Katika hatua nyingine, Meneja habari wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema mashabiki wa Simba msimu huu ni zamu yao kufurahi kwa kile ambacho timu hiyo wanaenda kukifanya.

Alisema wamefanya usajili mzuri na dalili nzuri imeonekana kwenye michezo waliyoicheza hivi karibuni ikiwemo ile ya Ngao ya jamii dhidi ya Yanga na Coastal Union.

“Kaka huu ni msimu wetu, tuna timu bora kuliko ile ya msimu uliopita, ujio wa mshambuliaji mpya unaenda kuchochea kitu kwenye timu yetu, msimu ujao utakuwa msimu wa kutamba kwa wana simba,“ alisema Ahmed.

Simba watafungua pazia la Ligi Kuu msimu wa 2024/2025 kwa kucheza na Tabora United kwenye uwanja wa Manispaa ya Kinondoni (KMC), jijini Dar es Salaam.

Michezo
Alhamisi Agosti 15, 2024
Nipashe

## Araujo ajiunga na Bournemouth

UKURASA 21



# Gamondi apania kumaliza kazi mchezo wa kwanza

### ●●●Awakomalia washambuliaji wake mazoezini, ataka umakini na kutumia kila....

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema anataka kuona kazi wanaimaliza kwenye mchezo wao wa kwanza hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vital'O ya Burundi utakaochezwa Jumamosi kwenye uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Akizungumza muda mfupi baada ya kumaliza mazoezi yao jana, kocha huyo alisema anataka kuona wanatumia kwa usahihi kila nafasi wanazozitengeneza ili kupata ushindi mnono utakaowapunguzia kazi kuelekea mchezo wao wa marudiano.

"Kama nilivyosema awali, hautakuwa mchezo mwepesi, lakini matamanio yangu ni kuona kazi tunaimaliza kwenye mchezo wetu wa kwanza, nataka twende kwenye mchezo wa marudiano tukiwa hatuna presha kubwa," alisema Gamondi.

Katika mazoezi yanayoendelea Kigamboni jijini Dar es Salaam kabla ya mchezo wa awali, Gamondi, juzi alikuwa makini mno na mkali kwa washambuliaji wake, Jean Baleke, Prince Dube, Kennedy Musonda na Clement Mzize akiwataka watumie nafasi zinazopatikana kupachika mabao upande wowote ambao mpira utakuwa, mguu wa kulia au wa kushoto.

Kitendo cha kocha huyo kuonesha kukomalia safu yake ya ushambuliaji hasa Mzize ni kutaka kuona wanatumia nafasi nyingi wanazozitengeneza katika eneo la hatari la wapinzani wao.

Tangu kuanza msimu huu, Yanga imeonekana tishio kwenye safu

INAENDELEA UK. 23



Kiungo wa Yanga, Duke Abuya (kulia) akiwania mpira na wachezaji wa Green Warriors wakati wa mchezo wa kirafiki juzi kwenye viwanja vya Avic Town, Yanga ilishinda mabao 4-1. **PICHA: YANGA**

## Fadlu awashusha presha mashabiki

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kumsajili mshambuliaji mpya Lionel Ateba, kocha wa Simba, Fadlu Davids, amewaondoa hofu mashabiki wa timu hiyo kuelekea kwenye msimu mpya wa Ligi Kuu na mashindano ya Kimataifa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Fadlu, alisema hana shaka na kikosi chake kufanya vizuri msimu huu kwa kuwa anakiandaa katika namna ya kupambana na kutoa burudani kwa mashabiki.

Alisema ujio wa mshambuliaji mpya kama alivyoomba utaongeza makali kwenye safu ya ushambuliaji na kuwataka mashabiki wa timu hiyo kusubiri ,mambo mazuri' ligi itakapoanza.

"Tunaendelea na maandalizi yetu, nina kikosi kizuri na ninaamini baada ya mfupi tutakuwa pale ninapotaka kikosi changu kiwe, nataka mpira wa kasi na wenye matokeo," alisema Fadlu.

Aidha, alisema kupatikana kwa mshambuliaji mpya ni jambo zuri kwa kuwa ataenda kuongeza makali kikosini na kumpa wigo mpaka wa kuchagua nani wa kuanza kulingana na mchezo husika.

"Nimeona ubora wa kila mchezaji, kazi ninayoimalizia ni ile kuona mifumo na mbinu yangu wanaishika na tunaenda pazuri pia kwenye jambo hili," alisema Fadlu.

Alisema hana hofu na timu yake na anafahamu atarejesha furaha

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >